ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishiri na Nne – Tarehe 18 Julai, 2012

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika *(Pandu Ameir Kificho)* Alisoma dua

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamkaribisha Katibu na leo tunawageni mbali mbali ambao wamefika katika ukumbi wetu ili kuja kuona shughuli zetu tunavyoendelea. Wageni wetu wa leo katika ukumbi wa juu pale ni makundi manne.

1. Kundi la kwanza ni wanafunzi wa Skuli ya Mwembeladu, Jimbo la Rahaleo jumla yao ni wanafunzi 38 na walimu wao 5.

2. Kundi la pili ni wanafunzi kutoka *Stone Town Center* Makadara Branch, vile vile kutoka Jimbo la Rahaleo. Jumla yao ni 10, nawaomba wanafunzi hao 10 nao wasimame kusalimiana na Waheshimiwa Wajumbe. Ahsante sana.

3. Kundi la tatu ni familia ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nao ni wanne karibuni sana.

4. Kundi la nne ni wanafunzi wa skuli muhimu sana ya Sekondari ya Mfenesini ya Mhe. Naibu Spika, ni wanafunzi 18 na walimu wao 2 nawaomba wasimame wale pale. Vijana pamoja na walimu wao karibuni sana. Waheshimiwa Wajumbe hao ndio wageni wetu wa leo.

Nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru wageni wote ambao mmehudhuria kuja kuona shughuli zetu kwa leo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 50

Usafi wa Soko la Darajani

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-
Soko Kuu la Zanzibar lilioko Mji Mkongwe liko katika hali mbaya sana ya uchafu kiasi cha kutishia usalama wa afya za wananchi kutokana na mazingira yanayofanyiwa shughuli za uuzaji wa vyakula vikiwemo nyama na samaki na pia kuitia aibu nchi yetu kwa wageni wanaotembelea sana soko hilo. Eneo hilo pia linalotumiwa na watu wengi lina upungufu mkubwa wa vyoo na vile vilivyopo vikishindwa kutunzwa na kuwekwa safi.

(a) Ni lini Baraza la Manispaa litachukua hatua ya kurudisha haiba na usafi wa soko hilo kwa kutuhakikishia kuna utaratibu unaoeleweka wa kuweka mazingira ya soko katika hali ya usafi.

(b) Kwa nini maeneo yanyotengezwa katika soko hilo yanapokamilika hunyang'anywa wachuuzi waliokuwa wakiyatumia kabla na badala yake kupewa watu wengine.

(c) Je, kuna mamlaka yoyote iliyowekwa na Baraza la Manispaa kusimamia uongozi na uendeshaji wa soko hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 50 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, Baraza la Manispaa tayari linachukua hatua madhubuti ya kuhakikisha kwamba Soko Kuu la Darajani linakuwa safi kwa kuzishishirikisha Kamati zake za madiwani za ustawi wa jamii na Kamati ya kazi za ujenzi na mazingira ambazo kamati hizo huwa zinafanya ziara ya kuelimisha wafanyabiashara wa Soko hilo katika kuimarisha na kutunza haduma ziliopo pamoja na usafi wa mazingira.

Mhe. Spika, aidha vikundi vya mazingira na Kamati ya Wafanyabiashara wa Soko la Darajani nao wanashajihishwa katika kushiriki kuliweka safi soko hilo. Sambamba na hayo Baraza la

Manispaa hivi sasa linaendelea na operesheni maalum za usafi na kupunguza msongamano wa wafanyabiashara na kuwekwa kwa utaratibu uliobora.

(b) Mhe. Spika, utaratibu wa matengenezo wa Soko la Darajani ni kwa njia za ubia yaani BOT. Kwa hivyo baada ya matengenezo wafanyabiashara waliopo wanalazimika kulipa ada kulingana na matengenezo yaliyofanyika. Kilichojitokeza kwa baadhi ya wafanyabiashara baada ya kupatiwa sehemu mpaya huwa wanakataa kulipa ada kwa mujibu wa mkataba wanaofunga na Baraza la Manispaa. Hali hii husababisha ukiukwaji wa taratibu za kimkataba na hivyo hulazimisha Baraza la Manispaa kuchukua hatua za kumpangisha mfanyabiashara mwengine.

(c) Mhe. Spika, hakuna mamlaka yoyote iliyowekwa na Baraza la Manispaa ya kusimamia Soko Kuu la Darajani, isipokuwa Baraza la Mainispa limemuweka Mkuu wa Soko na watendaji wa Manispaa ambao wanashirikiana na Kamati ya Wafanyabiashara wa soko hilo katika kusimamia utoaji wa huduma ukiwemo usafi wa mazingira pia kufuata taratibu za afya, kulipa ada na kusimamia madeni. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru Mhe. Spika, na namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba juhudi hizo anazozichukua Baraza la manispaa hazijazaa matunda yoyote ukizingatia eneo la soko hasa kwenye machinjio ya kuku na eneo linalouziwa nyama, pamoja na soko la samaki bado liko katika hali mbaya sana hasa katika lile eneo la kuuzia kuku na ukizingatia hata uuzaji wa nyama mpaka leo unafanyika kienyeji sana uchukuzi wake watu wanabeba kichwani hakuna hata vifaa vya kuhakikisha kwamba hakuna *contamination* baina ya mwili anayebeba na ile nyama ambayo inakwenda kuliwa na binaadamu. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba bado taratibu zake hazijaridhisha.

(b) Mhe. Spika, kuhususiana na maeneo ambayo hufanyiwa matengenezo na baadae kutokupewa aliyekuwa akiyatumia kabla

Mhe. Waziri katika majibu yake kasema kwamba inatokana na wachuuzi wenyewe kushindwa kulipa kodi baada ya matengenezo hayo. Mheshimiwa utakubaliana na mimi kwamba wapo wachuuzi katika eneo lililokuwa likiitwa Soko la ndizi ambalo mpaka leo nimekuwa nikiwasiliana na Baraza la Manispaa kutaka kupatiwa maeneo hayo lakini Baraza la Manispaa limekuwa likiwapiga chenga baada ya ahadi waliyowapa awali kwa sababu maeneo hayo wamepewa matajiri wengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza naomba nimjulishe Mhe. Ismail kwa mtizamo wangu wafanyakazi wa Manispaa waliokuwepo Marikiti wanajitahidi sana, lazima tuwapongeze kwa kiwango chao, kwa matatizo waliyonayo ya upungufu wa vifaa. Pale tuna shifti tatu zinazojishughulisha na usafi. Shifti ya kwanza inaingia asubuhi, tuna shifti nyengine inaingia mchana, na shifti nyengine inaingia jioni. Tunajumla ya wafanyakazi 17.

Tatizo liliopo na hili tunamuomba Mhe. Mwakilishi atusaiditie na yeye kwa vile ni Mwakilishi wa Mji Mkongwe ni watu kutokutii na kutokufuata taratibu zilizowekwa za kuuza biashara katika sehemu zinazotakiwa. Katoa mfano mzuri sana hapa katika Soko la Kuku kunasehemu panawekwa kuku na sehemu ambapo mbali kabisa na kuchinjia. Lakini leo ukienda pale pa kuchinjia hupajui, yaani pamezidiwa, watu na matenga yao na manini yao. Sasa ukijaribu kuwaondoa Mhe. Mwakilishi anakuja aah! Watu wangu hao, aste aste kidogo.

TAARIFA

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nimuombe Mhe. Waziri ni siku gani niliyomfuata kumwambia watu wangu awaondoe pale.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mheshimiwa hakuna siku maalum lakini nimeshazungumza nae mara nyingi Mhe. Jussa kuwa tusaidiane haya masuala, mara nyingi namfuata. Na yeye ndiye mwenye wananchi wa Mji Mkongwe hii dhamana na yeye hawezi kuiepuka yeye ndiye mwenye watu wa Mji Mkongwe.

Sisi tukifanya wajibu wetu yeye huwa anakinga kifua aaah! Watu wasiguswe. Sasa mimi naomba sana tushirikiane, tusaidiane, mle mwenye taratibu zifuatwe, msimokuwa na taratibu tushirikiane wale watu wasifanye kazi hizo, ni suala dogo sana. Lakini ikiwa tunaiwachia serikali tu na wewe mwakilishi tusaidie.

Mimi naomba sana muheshimiwa kuhusu upande wa pili suala la wauza ndizi, nakubali kweli pale walikuwepo wafanyabiashara kwenda kwa Shamsu, taarifa niliyonayo kwamba ni kweli, kuna baadhi kulikuwa na mizozo hawakuwahi kurejeshewa zile sehemu zao. Kubwa baada ya kuulizia nikaambiwa tatizo ndio hilo. Kwamba ule utaratibu walioweka wa BOT wao walishindwa kukubali kulipa ada kwa sababu zamani walikuwa hawalipi chochote. Sasa hizo ndio sababu nilizozipata.

Lakini mimi namuomba tena Mhe. Ismail Jussa, mimi na yeye nipo tayari tushirikiane tuwafuate hao watu, tutizame vipi tutaweza kulirekebisha suala hili.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:- Mhe. Spika, mahali popote au Soko lolote linahitajika wafanyakazi wa kutosha.

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi wanaoshughulika na usafi katika eneo lile la Darajani.

(b) Je, hao waliokuwepo wafanyakazi wanatosheleza kudumisha hali ya usafi katika Soko la Darajani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ujumla pale palikuwa na wafanyakazi 22 wanaoshughulika na usafi. Kwa bahati mbaya wamestaafu 5 hivi sasa tuna wafanyakazi 17. Kwa kweli tunakubali kwamba hawatoshi, tunakubali kwamba hawatoshi, lakini tupo katika kufanya mipango ili tuone tutalirekebisha vipi suala hili. Ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri, wapo wananchi wanaoleta samaki kutoka sehemu mbali mbali katika Soko la Darajani na watu wale huleta samaki wale ambao bado hawajapasuliwa na kutolewa machango, hutoa machango pale na kutia katika makaro na kuleta harufu katika mji ule.

Je, Mhe. Waziri, kuna utaratibu gani wa kuwafanyia watu hawa ili waweze kupasulia samaki katika sehemu ya baharini na machango kutupa katika bahari. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, soko la samaki Darajani pale ndani watu wote

wamejengewa vibaraza, wale wa ndani nasema na wale wanafuata taratibu, wakishakununua mnadani pale wanakwenda wanapasua na matumbo yale wanayaweka sehemu maalum. Tatizo liko kwa wale wa nje ndio pale niliposema ambapo nje si ruhusa kuuza samaki.

Ukenda jioni pale kuanzia saa 8, saa 10, kuanzia sokoni pale mpaka unakwenda jumba refu kama unakwenda zako mitaa ya Malindi pale utakuta wauza samaki wanapanga nje. Ndiyo yale niliyoyasema kwamba hakuna utaratibu wowote. Sasa wale tunajitahidi sana kuwaelimisha, kuwafahamisha, lakini matatizo tunayoyapata ata askari wetu wa Manispaa wanatishiwa kupigwa. Haya ndiyo matatizo tunayoyapata, tunajitahidi sana.

Naomba sana hili jukumu la kuweka mji wetu katika hali ya usafi, katika hali ya mazingira mazuri, hali ya kuvutia ni jukumu letu sote naomba tusaidiane. Taaluma sisi tunajitahidi kutoa naomba tusaidiane sana.

Nam. 188

Makondakta wa Daladala Kuwanyanyasa Wanafunzi wa Skuli

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Kny (Mhe. Mohammed Said Mohammed) – Aliuliza:-

Baadhi ya makondakta wa daladala wamezua mtindo wa kuwanyanyasa wanafunzi wa Zanzibar kwa kuwashusha ndani ya gari wanapotokea skuli. Jambo hili husababisha wanafunzi hao kuchelewa kurudi majumbani mwao hadi saa mbili za usiku.

Je, Serikali inachukua hatua gani ya kuwalinda wanafunzi hao ili wasinyanyasike zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 188 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba baadhi ya makondakta wa magari ya daladala wanaendelea kuwanyanyasa wanafunzi na serikali imechukua hatua kadhaa ikiwemo kuandaa kanuni za makondakta, kuandaa kanuni za abiria wakiwemo wanafunzi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni hizo ni kosa kwa kondakta kumnyanyasa mwanafunzi au abiria mwengine yoyote yule. Ikiwa atatiwa hatiani kwa kosa hilo, atalazimika kulipa faini isiyopungua dola 10 za Kimarekani.

Hivyo kwa kupitia Baraza lako tukufu naomba kuwakumbusha na kutoa wito kwa abiria wote ambae atafanyiwa kitendo chochote cha kunyanyaswa, apelike taarifa hiyo katika kituo cha polisi kilicho karibu naye kwa kutaja namari ya usajili wa gari ilyomfanyia vitendo hivyo ili kuona kwamba hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya mvunjaji huyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Waziri kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Spika, swali hili ni la muda mrefu sana na kila siku tunapiga kelele juu ya daladala kuwahangaisha wanafunzi. Kwa kuwa suala hili bado halijapata ufumbuzi pamoja na serikali kutoa kauli kama hiyo.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri, je, ni madereva wangapi wa daladala na makonda wao ambao wametiwa hatiani kutokana na suala hili. Kama bado hawajatiwa hatiani kwa nini Wizara yake ikawa haijawatia na wakati suala hili linaendelea kuwa sugu na wao hawasikii kwa kuambiwa kwa maneno tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi anachotaka kujua ni hatua gani ambazo zimechukuliwa dhidi ya wale ambao wanaendeleza kufanya kosa hili. Tumeeleza kwamba kitendo cha kumnyanyasa abiria akiwemo mwanafunzi ni kosa kwa mujibu wa sheria. Sisi wajibu wetu ni kusimamia sheria. Wajibu wa polisi ni kufanikisha au kutekeza sheria.

Mhe. Spika, namthibitishia Mhe. Mwakilishi, ni watu wengi madereva na makondakta wao ambao wameadhibiwa chini ya sheria hii ambao walifanya makosa hayo tunayoyasema. Jambo la msingi ni kuamua na kuarifu wananchi wetu kwamba ukitendewa kosa ufate utaratibu wa kufikisha taarifa katika sehemu husika ili vyombo vinavyohusika kutekeleza hiyo sheria iliyovunjwa viweze kuchukua hatua.

Sisi kama wizara wajibu wetu ni kusimamia lakini ili kusimamia vizuri ni lazima tupate taarifa na taarifa hizo tunavyozipata ni lazima tushirikiane na wenzetu na jeshi la polisi ili kuona zile hatua zinazostahiki zinachukuliwa ikiwa kama ni suala la kumfikisha Mahakamani na kulipa faini. Bila ya kutoa ushirikiano huo tutaendelea kulalama na hatua hazitochukuliwa na vitendo vitazidi.

Imani yangu kwamba kama wananchi watahamasika kwa kuona kwamba wametendewa vitendo ambavyo ni vya kunyanyaswa au vipo kinyume na taratibu na sheria na akifika katika vituo vya polisi basi mimi naamini kwamba jambo hili litapungua kwa kiasi kikubwa. Kwa hivyo ni idadi kubwa ya watu ambao wameshachukuliwa hatua hizo. Naomba tena tuendelee na muamko wa kufikisha taarifa hizi katika vituo vya polisi ili kuona kwamba sheria inatakelezwa kama inavyotaka.

Mhe. Salimin Awadh Salimin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa suala la msingi limezungumzia zaidi ya kuwanyanyasa wanafunzi. Na kwa kuwa wanafunzi wanaonyanyaswa asilimia kubwa ni watoto wadogo ambao wakati mwengine wanaondolewa kwenye mabao na kuwekwa chini. Lakini Mhe. Waziri alivyokuwa anajibu suala amesema wanaonyanyaswa basi warikodi nambari ya magari na kwenda kituo cha polisi.

(a) Atakubaliana nami kwamba watoto wale wadogo hawana uwezo wa kurikodi namba za gari halafu kwenda kushtaki polisi.

(b) Ni hatua gani sasa atazichukua juu ya madereva wale ambao wanawanyanyasa watoto wadogo katika kupata usafiri wa kwenda skuli. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika,

(a) Nakubaliana na taarifa ya Mhe. Mwakilishi kwamba watoto wadogo hawatokuwa na uwezo kurikodi, lakini imani yangu kwamba hiyo gari watakayoipanda kuna watu wazima na watu wazima ndio walezi wa hao watoto wadogo. Sasa kama mtu mzima yumo ndani ya gari amemuona mtoto amenyanyaswa, basi yeye amsaidie huyo mtoto kuchukua hizo taarifa kupeleka kituo cha polisi ili sasa kuona polisi wanatekeleza hatua zinazofuata.

Mimi naamini kama mtoto mdogo ni kweli hawezi kufahamu hizo taratibu lakini watu wazima waliokuwemo ndani ya daladala wawasaidie hao watoto, kuchukua hizo taarifa kupeleka kituo cha polisi na huo ndio wajibu wa jamii, kusaidia kuilea jamii ya watoto wadogo. Sasa kama mtoto mdogo hawezi kufanya hilo jambo basi watu wazima waliokuwemo ndani ya gari ile wachukue hatua ya

kuwasaidia watoto ili kwa kutambua akimsaidia mtoto wa mwenzake na mtoto wake atasaidiwa.

(b) Hatua zinazochukuliwa ni zile zile kwa mujibu wa sheria ilivyo, kwamba kama wametenda kosa, tutazuia leseni yake, tutafuta leseni yake, ndio sheria inavyoelekeza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali lifuatalo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri, suala la msingi limezungumzia kwamba watoto wanapoteremshwa katika magari wakati mwengine hufika usiku hawajafika majumbani kwao. Na kwa kuwa katika kujali hili sisi hapa Baraza la Wawakilishi serikali ilipitisha Mswada wa kumlinda mtoto kwa kiasi kikubwa sana. Na kwa kuwa tulisema atakaegundulikana na suala hili la kumnyanyasa mtoto atalipa dola 10 za Kimarekani ambazo kwa kweli ni kama TSh 16,000/-
.

(a) Je, kwa kuwa sisi tumepitisha Mswada wa kumlinda mtoto, haoni kwamba adhabu hii ni ndogo.

(b) Ni lini serikali itafikiria kubadilisha adhabu hii na kuzuia leseni pamoja na gari kuizuilia shughuli za biashara.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, mimi naomba kidogo tu tuelezane kama tunachokizungumzia hapa ni suala la mtoto kunyanyaswa. Miongoni mwa manyanyaso ambayo ananyanyaswa mtoto ni kuona kwamba amekaa kwenye kiti anaondoshwa anakaa kwenye deki, anayemuondosha ni mtu mzima. Maana yule mtoto amekaa kwenye kiti anaondoshwa mtoto anakaa mtu mzima. Basi na sisi watu wazima tujenge imani kwamba aaaah, wewe mtoto endelea kukaa kama nafasi haimo ushuke usubiri gari nyengine.

Lakini ikiwa wewe mtu mzima unashiriki kumuondoa mtoto katika kiti yeye aweko deki halafu unalalama.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Katika suala la msingi amesema kwamba wanapoteremshwa watoto katika gari hufika usiku hajafika majumbani kwao hapo. Sio kuondoshwa katika benchi na kuwekwa kwenye deki. Ninachozungumzia kushushwa kwenye gari na kusababisha kufika usiku, jambo ambalo linaweza kupelekea mpaka kesi za ubakaji kwa wanafunzi wetu. Hilo ndilo nililolikusudia Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, mimi ndio nilikuwa najibu naomba Mhe. Mwakilishi ananikatisha. Yeye ameniuliza na mimi ndio nataka kumjibu. Vyenginevyo kama ana majibu ya kuandika anambie, mimi najibu kile ninachoelewa sasa asinikatishe.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wanafunzi hawa tunaowazungumzia wana nyakati tofauti. Ikiwa huyo mwanafunzi wenyewe huo muda aliokwenda kusubiri gari ni saa 12, tunategemea atafika nyumbani saa ngapi. Maana kama wewe umekwenda kituo cha daladala saa 12:30 unategemea utafika nyumbani muda gani. Lakini msingi mkubwa mimi ninachokiomba ni ushirikiano. Hayo magari ya abiria hakuna gari inayopakia watoto peke yake, wamo watu wazima na hao watu wazima ndio wajenge huo msingi wa kuwasaidia hao watoto.

Suala la adhabu kwa mujibu wa sheria hii Sheria nambari 7 ya mwaka 2003 chini ya Kifungu cha 80 kimempa mamlaka Mhe. Waziri anayehusiana na masuala ya usafiri kutoa *regulation*. Naamini kama adhabu hiyo ni ndogo tutamuomba Mhe. Waziri alizingatie hilo ili kuona kwamba hatua stahiki kwa adhabu inayostahiki kwa watendaji wa makosa haya inachukuliwa.

Nam. 190

Abiria Wanaosafiri kwa Ndege Kutokupewa Kitu cha Kula

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:-

Hapo siku za nyuma wasafiri wa ndege walikuwa wnapewa pipi au kitu cha kula ili kuufanya mdomo uwe katika mazoezi ya kuhangaika au kuchakuwa chakuwa. Huduma hizi zilitolewa bure na ongozi wa ndege husika. Pamoja na hayo uchunguzi wa kisanyansi unaonesha kuwa, zoezi kama hili ni muhimu kwani kuondosha kuziba kwa masikio. Huduma hizi zilitolewa bure na uongozi wa ndege huzika.

(a) Je, ni sahihi kwamba kutokuwapatia chochote abiria wakati ndege ikiwa katika safari zake kunaweza kukasababisha matatizo kwa abiria hao.

(b) Ikiwa uongozi wa ndege ndio dhamana wa hilo na kama umeshindwa kutoa huduma hiyo, kwa nini uongozi wa ndege usitoe taarifa mapema kwa abiria ili wajihadhari wenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali nambari 190 vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo. Suala la huduma hizi anazozungumzia Mhe. Mwakilishi, hazina nasaba ya moja kwa moja na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Sisi kama Mamlaka tunachotakiwa zaidi ni kujikita katika ulinzi na usalama kwa maeneo yote ya uwanja wetu. Hata hivyo katika eneo hilo sambamba na suala la huduma bora nalo pia tunalazimika kulisimamia yaani *(Safety, Security and Facilitation).* Ili kufanikisha hilo tunalazimika kuona kwamba watumiaji wote wanafuata taratibu tulizojiwekea ambazo zinaendana na masharti ya TCCA pamoja na ICAO.

Mhe. Spika, kikawaida ndege inaporuka zaidi ya futi 7,000 kutoka usawa wa bahari wakaki ikiwa inajiandaa kutuwa humpelekea abiria aliyomo kupata athari za muinuko unapokuwa juu kwa umbali mkubwa kutoka usawa wa bahari (*Due the height from the sea level)* mwili na hasa masikio yanapata usumbufu pale tu unaposhuka pamoja na mapigo ya moyo kubadilika kwa ujumla. Tabaan suala la mfumo wa pumzi yaani suala la kupumua nalo huwa linabadilika na kuathirika.

Aidha ili kukabiliana na usumbufu huo ndio hapo anaposhauriwa abiria ni vyema akawa anafumbua mdomo ili kuruhusu mabadiliko hayo ya (*height*) yasimuathiri zaidi.

Katika hatua kama hiyo ndio maana suala hilo mashirika yakajenga utaratibu wa kugawa pipi au mibani za kutafuna, ili kuondoa usumbufu huo. Hata hivyo, kwa ujumla jambo lenyewe ni la wakati maalum, tunawaomba wenzetu wamiliki wa mashirika waendelee na utaratibu huo.

Baada ya melezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, si sahihi kwamba kutowapatia chochote cha kutafuna kutapelekea matatizo au athari kwa abiria hao. Jambo la msingi ni kutoa elimu kwa abiria, ili afahamu jambo lenyewe. Hata hivyo, kuwapatia kitu kama hicho kunaweza kuondoa malalamiko yaliopo.

(b) Tunaomba wahusika hasa uongozi wa mashirika walisimamie hilo na matarajio yetu ni kwamba suala la kuwapatia elimu wasafiri litaweza kusaidia sana kwa abiria wetu kulielewa tatizo lenyewe

pamoja na njia ya kukabiliana nalo. Jambo la faraja ni kwamba hata maji yanasaidia sana kwa athari tulizozitaja, ingawa abiria wetu wamekuwa hawayatumii, pamoja na kuwa yanapatikana katika ndege zetu zote, pengine tatizo kubwa ni kutokuelewa athari za tatizo lenyewe lilivyo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kwa kuwa ndege inaporuka rubani wa ndege hutoa taarifa kwamba, inapotokea ajali mlango wa kulia au kushoto ndio wa kutokea na *life jacket* iko katika kiti.

Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba, inapotokea ajali mtu huyo ni wakati gani atavaa koti lile. Hivyo, huoni kwamba kuweka utaratibu wa kuvalishwa koti kama vile mtu anapoingia katika boti, ili kupunguza ajali itakapotokea mtu yule awe tayari ameshavalishwa lile koti ahsante?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, utaratibu ule ndio ulioelekezwa na kikao na ndege zote duniani ndio utaratibu ambao unaofuatwa, kwamba unapanda kwenye ndege na kuelekezwa *life jacket* lipo wapi na inapotokea athari ni wajibu wa rubani kukuelekeza namna ya kuvaa, ili kuweza kujiokoa.

Miongoni mwa matatizo yaliomo ni kwamba ukilivaa jacket lile ndani ya ndege huwezi kutoka na unapotakiwa wakati unatoka ndio uvae, hivyo ndivyo taratibu za kikao zilivyoelekeza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alisema Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kazi yake hasa ni kusimamia usalama kuliko kuhakikisha watu wanapata pipi na ubani.

Sasa mimi naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwamba katika kusimamia usalama moja katika kanuni zetu ni kuwa ndege zote ambazo zinachukua abiria zinatakiwa kuwa na *pilot* na *core pilot*. Lakini ndege zetu nyingi ambazo zinatoa huduma ndogo ndogo hapa hasa zile za baina ya Dar-es-Salaam na Unguja, pia Pemba na Unguja unakuta kwamba zinakuwa na *pilot* mmoja, kwa hiyo ni binadamu na kilitokea lolote hakuna hatua zozote zinazoweza kufanyika, ili kuhakikisha usalama wanapatiwa.

Kwa nini Mamlaka ya Viwanja vya inayosimamiwa na wizara yake inashindwa kusimamia Kanuni hii ya msingi ambayo inataka kuwe na *pilot* wawili katika ndege zinazobeba abiria?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, utaratibu wa kurusha ndege ni utaratibu ambao unaoendana na masharti pamoja na Sheria za Kimataifa. Kwa hivyo, analolisema Mhe. Mwakilishi ni kweli, lakini utaratibu ulivyo, kwamba ndege yoyote ambayo uzito wake utakuwepo chini au si zaidi ya 12500 *pounds* inaruhusiwa kurushwa na *pilot* mmoja na ndege ambayo itakayokuwa imezidi uzito huo, basi inalazimika kuwa na *core pilot*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndege nyingi hizi ambazo zinazosafiri Unguja, Pemba ziko *less* au *between* ya huo uzito wa 12500 *pounds*. Kwa msingi huo bado utaratibu haujakiukwa na watendaji hao wanakwenda kwa mujibu wa sheria zilivyo.

Mhe. Spika, ikifika pahala kwamba uzito huu tunaueleza umezidi basi tutawalazimisha *pilots* na mashirika yao kufuata taratibu hizi za kimataifa, ili kunusuru maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo. Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar inaitaka serikali yetu kulinda raia na mali zao na kwa kuwa Sheria za Kimataifa zinafafanua jinsi ya ndege ya kurushwa kwa rubani mmoja na wawili. Kwa kuwa msingi wa nchi ni Katiba, je Mhe. Waziri haoni kwamba ndege hizo zenye rubani mmoja hazifai, ili kwenda sambamba na matakwa ya Katiba? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, mimi nilichokieleza ni utaratibu wa Kimataifa, kwamba ndege inapokuwa na uzito huu inalazimika kuwa na rubani huyu na ikizidi uzito huu inalazimika kuwa na *core pilot*.

Lakini jambo kubwa utaratibu wa ndege ni usafiri ambao unahitaji taaluma, yaani ni usafiri ambao unahitaji ufuate taratibu zake na usafiri huu tunaouzungumzia ndio usafiri tunaoutumia. Jambo la msingi ni kuona kwamba zile taratibu zilizopo zinafuatwa.

Sasa tunaposema kwamba usafiri huu wa ndege ndogo haufai na wala mimi siamini, kwamba sababu huko zinakotengenezwa zinarushwa na kufika hapa na kuzitumia na wala hakujatokea athari. Mhe. Spika, mimi nadhani jambo kubwa ni kuhakikisha kwamba utaratibu uliopo wa kimataifa unafuatwa, pale ambapo utaratibu haufuatwi basi msingi ni wajibu wetu kukumbushana na kuona kwamba tunawarejesha wenzetu katika mstari uliopo.

Mhe. Spika, suala la *single pilot*, kima cha kuruka urefu, *cabin crew*, yote yanakwenda kwa mujibu wa idadi ya namba na ukubwa wa ndege yenyewe,

sio kwamba kila kitu kinafanywa kabla ya chenzake. Kwa mfano, ndege ili iwe na *crew* basi inalazika iwe na idadi maalum ya abiria ndio iingize *crew*, pia ndege ili iwe na *core pilot* inalazimika iwe na uzito maalum kwa ajili ya kufanya hivyo.

Kwa maana hiyo, yote haya yanayokwenda yanakwenda kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Kimataifa na wala hakuna sehemu ambayo imekiukwa utaratibu wowote katika urushaji wa ndege husika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, tunakushukuru. Tunaendelea.

Nam. 131

Ukosefu wa Jengo la *ZSTC* Tawi la Dar-es-Salaam

Mhe. Bikame Yussuf Hamad – Aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la *ZSTC* Tawi la Dar-es-Salaam limelazimika kukodi jengo la ofisi tangu mwaka 1970 hadi leo hii. Kwa kuwa gharama za kukodi zinaongezeka hadi kufikia milioni 31.0 kwa mwaka ukilinganisha na siku za nyuma jambo ambalo linapelekea kugharimu fedha nyingi kwa shirika hilo na kukosa faida nzuri.

Je, ni lini hasa serikali itafikiria kulinunua kabisa jengo hilo, ili kulipunguzia mzigo wa kodi shirika hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 131 linalohusiana na ununuzi wa jengo la *ZSTC* lilioko Dar-es-Salaam kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli ipo haja ya kulinunua jengo hilo ambalo liko Ilala lenye nambari 2-619-20148, ili kupunguza gharama za kodi inayoongezeka kila mwaka. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kulitambua hilo Mhe. Spika, tayari imeshachukua hatua ya kuomba kuuziwa jengo hilo mnamo mwezi wa Machi, 2010 na kukumbushia tena maombi hayo kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi Tanzania Bara, kwa barua ya tarehe 22 Oktoba, 2010 yenye kumbukumbu Nam. WUBU/M.120/C.6 VOL.11/181.

Aidha Mhe. Spika, wizara imewasiliana pia na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia Masuala ya Muungano, ili iweze kufuatilia kwa karibu ombi letu hili.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi. Kwa kuwa barua hiyo inawezekana isiwe ya mwanzo kwa sababu katika kipindi chote cha miaka mitano ya mwanzo tuliyokuwemo katika Baraza hili nilikuwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi na tulikuwa tunafuatilia kuhusu jengo hilo. Je, ni kikwazo gani hasa kilichopelekea kwamba mpaka leo ikawa jengo hilo halijapata kununuliwa au ikiwa halinunuliki tena, kwa nini wizara inaling'ang'ania kukodi na kuweza kutafuta eneo jengine na kujenga.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli kwamba inawezekana ni muda mrefu suala hili limekuwa likifuatiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini bado hatua zimekuwa hazijaonekana kuchukuliwa.

Lakini naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kufuatana na kutokuchukuliwa hatua huko, hivi sasa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tayari ameshachukua hatua za kutaka kuwasiliana na uongozi wa Wizara kama hii inayohusika huko Bara, ili waone katika ngazi za juu za kitaifa wanaweza kutusaidia vipi katika kulitatua tatizo hili.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, tunakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Nam. 183

Ugonjwa wa Kansa na Kifafa

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad (Kny: Mhe. Mohammed Said Mohammed) – Aliuliza:-

Ugonjwa wa kansa na kifafa ni miongoni mwa magonjwa sugu yanayowasumbua wananchi wa rika zote.

(a) Je, serikali inawatumiaje wanasayansi tulionao kuchunguza asili na suluhisho la maradhi hayo?

(b) Je, ni kweli kwamba watafiti wetu wameshindwa kupata tiba ya maradhi hayo au hawajawezeshwa kufanya utafiti wa dhati?

(c) Je, kwa nini wagonjwa wa magonjwa hayo na wao wasipelekwe nje ya nchi kama wagonjwa wa magonjwa mengine yanayoshindikana?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 183 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kansa na kifafa ni maradhi ya zamani tena ni sugu ambayo yanasababu nyingi na zinazotofautiana. Hapa Zanzibar tunao madaktari ambao wanaofanyakazi na kuchunguza, kutambua na wanapoweza kutoa tiba sahihi ya saratani na kifafa wanatoa. Kutokana na sababu nyingi za matatizo hayo, hata nchi zilizoendelea huwa zina wataalamu ambao wanashughulikia tafiti tu za saratani na kifafa.

Kwa kweli watafiti ulimwenguni kote mpaka leo sababu nyingi za saratani na kifafa bado hazijulikani vizuri. Lakini kwa hapa Zanzibar wanasayansi ambao wanaofanya utafiti wa maradhi tu hatuna. Kwa hivyo, sio hapa tu, isipokuwa ulimwenguni tatizo hilo halijapata ufumbuzi.

Mhe. Spika, naomba kueleza utaratibu wa utibabu wa maradhi hayo hufanyika hapa kwa yale yanayowezekana na ikishindikana kabisa wanapelekwa nchi za nje kwa ajili ya matibabu zaidi.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wagonjwa hawa wa kifafa hapa wapo na wanapokwenda hospitalini wanaambiwa waende Dar-es-Salaam. Je, serikali inawasaidia vipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba kwa yale maradhi yasiyowezekana hapa Zanzibar yanapelekwa nchi za nje na katika sehemu ambazo wanazopelekwa ni Dar-es-Salaam. Kwa kweli wanapelekwa kwa sababu maalum, kwa mfano kuna baadhi ya vifaa hapa havipo kwa hiyo wanakwenda kupelekwa kule kwa ajili ya kupimwa na kurudi.

Mhe. Spika, kwa utaratibu wagonjwa wale wanatakiwa wapitie Bodi ya Afya, ambako wanachekiwa na halafu ndipo wanapopelekwa Wizara ya Afya kwa ajili ya kufanyiwa makisio ya kuweza kupewa nauli ya kufika kule pamoja na mtu wa kuwasindikiza.

Lakini si mara nyingi wazee wa watoto au wagonjwa hao huwa wanafuata utaratibu huo na mara nyengine huwa wanaharaka, kwa hiyo wanapewa vyeti vyao na kwenda wao wenyewe. Utaratibu wanatakiwa wapitie *Medical Board*, baadaye wapitie Wizara ya Afya kwa ajili ya kufanyiwa makisio na

ndipo wapelekwe. Kwa hivyo, wako ambao wanaotibiwa kwa kupitia hivyo pia wapo ambao wanaokwenda wao wenyewe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwanza niruhusu nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa jinsi alivyopendaza na style zake. Vile vile niipongeze serikali kwa hatua iliyochukua ya kuja na mpango hatimaye wa kujenga Kituo pale katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja ambacho kitashughulikia maradhi kama haya ya kansa.

Swali langu ni kwamba katika kipindi hichi ambacho bado hatua hiyo haijakamilika, wagonjwa wa kansa wanaendelea kuongezeka kila siku Zanzibar na wanaotibiwa Dar-es-Salaam katika Hospitali ya *Ocean Road* kumekuwa na gharama kubwa. Kwa mfano, mimi mwenyewe Mhe. Spika, nimewahi kupata uzoefu huo, kwa sababu niliwahi kutibu mgonjwa pale.

Sasa naomba kuiuliza wizara kwamba mbali ya kuwapeleka nje ya Tanzania kwa wale wanaohudumiwa pale Dar-es-Salaam tu. Je, serikali imekuwa na mpango gani kupitia Wizara ya Afya kuwasaidia wagonjwa ambao wengi hali zao ni masikini na inajulikana kwamba matibabu ya kansa yanakuwa na gharama kubwa sana?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli hayo anayoyasema Mhe. Mwakilishi, kwamba maradhi yanaongezeka. Kwa hivyo, ndio maana hivi sasa kuna Kitengo Maalum ambacho kimeundwa kwa ajili ya shughuli hizo, yaani ni hivi karibuni tu kimefunguliwa. Kwa kweli maradhi ni mengi na wengi wao wanapaswa kwenda Dar-es-Salaam kwa ajili ya matibabu, kwa sababu hapa ndio kwanza tunajiandaa na bado hatujafungua kitengo hicho.

Lakini maradhi ya kansa kama tunavyosema ni maradhi sugu tena ni ya muda mrefu. Kwa hiyo, mara nyengine mgonjwa anakwenda katika *Medical Board* na kusaidiwa, lakini sio kitu ambacho kitakachowezekana kwa kila mgonjwa anapokwenda Dar-es-Salaam, kwa sababu wanakwenda mara nyingi nap engine hata maisha yao.

Kwa mfano, mtu anaugua miaka 30 na kama Mwenyezi Mungu akimjaalia kuwa hai mpaka miaka 60, basi kila mwaka au hata inawezekana kila baada ya miezi sita ama mitatu anatakiwa kufika *Ocean Road Hospital*.

Kwa maana hiyo, wagonjwa wanaosafirishwa nje ni wengi, pengine tumemudu mara moja au mbili kumpa nauli yeye akaenda, lakini wagonjwa wengine nao pia wanatakiwa kupata fursa ile, hiyo na wale wagonjwa wengine wapya wanaokuja wanapewa fursa ile.

Lakini Kitengo cha Kansa cha Dar-es-Salaam wao wanatakiwa watoe matibabu bure, mara nyingi wakifika kule si aghalabu kupata dawa zote na hivyo inabidi wanunue na wanapoambiwa kununua wanashindwa na wanarudi hapa kwa sababu wanashindwa. Kwa hivyo, inabidi sisi kama jamii na kwa kweli wao kumudu maisha yote kununua dawa za kule ni gharama na wala hawataweza.

Sasa kitu ambacho kitakachoweza kutukomboa tu ni kuhakikisha kwamba hapa tunafungua kitengo, kwa ajili ya kuweza kuwatibu wagonjwa wetu hapa hapa. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri katika swali la msingi aliulizia maradhi ya kansa na kifafa.

Sasa mimi naomba kidogo niulizie kuhusu kifafa, kwa sababu kwa mujibu wa taarifa tulizonazo, kifafa mara nyingi ni tatizo ambalo limo katika kichwa (*brain*). Kwa kuwa katika nchi yetu tunalo tatizo la hawa wataalamu katika mambo ya akili na ubongo tangu alipostaafu Dkt. Wakili na kwa mujibu tulivyoelezwa kwenye bajeti ni wataalamu wawili tu ambao wame-*specialise* mambo hayo ambao wako masomoni na bado hawajamaliza masomo.

(a) Je, ni lini Mhe. Waziri wizara yake itawashawishi hawa vijana wanaomaliza *degree* ya mwanzo kuchukua hii *Profession* ya *Psychiatrist*, ili kupunguza tatizo la wagonjwa wa kifafa katika nchi yetu?

(b) Kwa kuwa wagonjwa wa saratani mara nyingi tunakimbilia Dar-es-Salaam katika *Ocean Road Hospital*, kwa ajili ya kutiwa mionzi pamoja na matibabu mengine. Kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na kuongezeka hewa ukaa katika hewa, uwezekano wa wagonjwa wa saratani katika nchi hii ni kuongezeka sana.

Je, Mhe. Waziri hivi ni lini wizara yake itafikiria angalau ile *preliminary treatment* ya haya mambo ya kansa kufanyika hapa *Mnazimmoja Hospital*, ili kutupunguzia adha ya kwenda Muhimbili na huku uwezo hatuna, *Yailahi Yarabi Toba*?

Mhe. Naibu Waziri: Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Mwakilishi anazungumzia kuhusu wataalamu wa afya, nafikiri kila tukikaa hapa tunachozungumza ni upungufu wa wataalamu wa afya ndio changamoto yetu kubwa.

Kwa kweli mimi tangu nimeingia Wizara ya Afya, hao madaktari walioko huku ni madaktari wa sita wanaosomeshwa somo hilo. Wanne wengine na mmoja akiwemo Dkt. Wakili wamesomeshwa na Dkt. Wakili ameamua kustaafu kabla ya wakati kwa sababu anazozijua yeye mwenyewe na wengine wameondoka. Kwa hivyo, tunasomesha wengine, yaani wanapoondoka tunasomesha wengine.

Hata hivyo, si madaktari wanaohusika na hilo kwenye matibabu na *nurses* pia wapo, kwa kweli tunao *nurses* wengi ambao wanaweza kuwahudumia wagonjwa hao. Mhe. Spika hivi sasa yupo Mcuba pale na yeye anashiriki kufanya hivyo pia kuna madaktari wengi tu ambao wanaokuja na kuondoka wanaokuwepo *Mental Hospital*.

Kwa hivyo, wagonjwa waliopo hivi sasa sio kwamba wana-*safer* sana kwa sababu ya kukosa madaktari au huduma. Lakini hao wawili watakapokuja ndipo tutakapokuwa na madaktari sisi wenyewe na tutajitahidi kuendelea kusomesha wengine.

Mhe. Spika, kama tunavyosema kwamba madaktari wanachotaka kukisoma ni uamuzi wao, kwa sababu tunaweza kuwashajihisha kama mtu jambo halitaki basi hasomi.

Kwa hiyo, tumuombe Mwenyezi Mungu na nimuombe Mhe. Mjumbe kama anaye mtoto amshajihishe asome na baadaye mimi nije nimpeleke akasome labda itatusaidia, yaani amshajihishe mwanawe asome apate na awe daktari na halafu amwambie mwanangu nataka ukasome *Psychiatrist*, aone atakavyoweza kuipata shida kama halitaki hilo somo. Kutokana na hali hiyo, tunajaribu na tunaowapata tunawapeleka na hilo la kwanza.

Kuhusu suala la matibabu ya kansa. Kwa kweli matibabu yako ya aina nyingi, kwa sababu kuligundua peke yake ni tibabu kwa sababu tayari umeshajua tatizo. Lakini kuna matibabu ya *operation* hapa tunayafanya, kuna matibabu ya kuwawekea dawa ambayo yanafanyika kila mwezi hapa tunayafanya na linapokuja suala la mionzi, mashine hapa hatuna ndipo tunapowapeleka Dar-es-Salaam.

Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kujibu mwanzo kwamba Kitengo cha Kansa kitafunguliwa Mnazimmoja Hospital kama ni sehemu ya rufaa na ni matumaini yetu wakati huo yale yote yanayohitajika kwa ajili ya matibabu hayo yatapatikana hapo. Kwa hivyo, tumuombe Mwenyezi Mungu atuweke hai, ili hilo lifanikiwe.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, tunakushukuru. Tunaendelea.

Nam. 126

Elimu Juu ya Haki za Watoto

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Katika taarifa ya mwaka 2007/2008 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora sehemu ya (Matokeo ya Utafiti) imegundua kwamba kuna uwelewa mdogo sana wa Haki za Watoto.

Je, serikali haioni kama kuna haja ya kutoa elimu katika sehemu zilizobainika kutosimamiwa vyema Haki za Watoto kama sokoni na sehemu nyengine tofauti?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto) – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 126 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2007/2008 ilionesha kuwepo kwa uelewa mdogo wa Haki za Watoto. Hata hivyo, kuhusu Haki za Watoto tulikuwa tukizitoa na kuzieleza katika maeneo tofauti ya hapa Zanzibar, zikiwemo:-

- Shehia kupitia Mabaraza ya Watoto.
- Maeneo ya Mikutano ya Wanajamii wenyewe.
- Kupitia Mikutano ya Kisekta na Warsha.
- Vyombo vya Habari.

Vile vile taaluma hiyo tunaendelea kuitoa.

Aidha ni vyema Mhe. Mwakilishi aelewe kwamba wale wanaokiuka Haki za Watoto katika maeneo ya masoko wanatoka katika jamii ambako wizara ndio inajikita katika utoaji wa elimu kuhusu Haki hizo za Watoto.

Mhe. Spika, pia ni vyema tukaelewa kwamba moja ya majukumu yetu sisi Wawakilishi ni kuelimisha wananchi wetu katika majimbo yetu, mambo mbali yanayohusu uchumi, siasa na jamii likiwemo suala zima la Haki za Watoto na namna tunavyotakiwa sisi wazee kuwalinda na kuwatetea watoto hao haki zao.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na juhudi zote ambazo wanazichukua katika kuelimisha, lakini umasikini ndio unaopelekea watoto hawa kutafuta ajira hizo. Je, serikali itachukua hatua gani juu ya kuondoa tatizo hilo?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, kweli umasikini ndio unaoleta matatizo haya. Lakini naamini Mhe. Mwakilishi anajua kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi katika miradi mbali mbali ya kuondoa umasikini huo.

Kwa hivyo, ni matumaini yangu kuwa Mhe. Mwakilishi pamoja na jamii watajiunga katika vikundi ambavyo vinasaidiwa kwenye miradi mbali mbali ya serikali, ili kuweza angalau kutatua matatizo hayo ya umasikini, ambayo *indirectly* itawasaidia watoto wetu kutokufanyakazi ambazo hazistahiki kisheria.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Kwa kuwa watoto wanayo haki ya kujua wajibu huu wa haki zao na kwa kuwa elimu hii pamoja na kwamba Mhe. Waziri amesema kuwa wanatoa, lakini kuna kuwa na siku maalum ya kujua kama Siku hii ni ya Mtoto wa Afrika au Ulimwengu.

Je, siku hii inajulikana kutokana na watu walioko mjini tu, hivi wizara yake itafanya jitihada gani ya kuwaelimisha watoto, ili wajue mpaka vijijini kama leo ni Siku ya Mtoto na wao wajue kama leo ni Siku ya Mtoto Duniani?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, hili ni suala zuri naahidi kwamba wizara yangu itajitahidi kushajihisha wananchi na kabla Siku hiyo ya Watoto Duniani au Afrika, basi taarifa tutaitoa katika vyombo vya habari kwamba siku kadhaa ni sherehe au ni Siku ya Watoto na hiyo tutaieneza katika wilaya zote, ambapo watoto na wao watapata taarifa kwamba ni siku yao na wao waweze kutoa michango yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, tunakushukuru. Tunaendelea.

Nam. 63

Fedha Kuhifadhiwa Majumbani Pemba

Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Mnamo mwezi wa Aprili mwaka huu Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein ametoa wito kwa wakulima wa karafuu wasihifadhi fedha majumbani kwa sababu za kiusalama.

(a) Je, taasisi za fedha zimechukua hatua gani za kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutumia huduma za Benki?

(b) Kwa kuwa serikali imetumia bilioni 71 kununua zao la karafuu na Kisiwa cha Pemba kunufaika na zaidi ya bilioni 63. Kwa nini mzunguko wa fedga katika mabenki bado ni mdogo Kisiwani humo licha ya fedha nyingi kutumika kununua zao hilo?

(c) Ofisi hii ina mpango gani wa kufanya utafiti wa kujua kwa nini mzunguko wa fedha haupo na fedha hizo kushindwa kunufaisha sekta nyengine za biashara kisiwani humo?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Taasisi za Fedha hasa Benki ya Watu wa Zanzibar na *NMB* wakishirikiana na *ZSTC* wamezipitia kambi za wananchi, ambao wanachuma karafuu, pia wamezipitia sehemu za kuuzia karafuu pamoja na wauzaji wa karafuu katika maeneo yao wanayoishi kwa lengo la kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kutumia huduma za benki. Vile vile wizara iliyopewa dhamana ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na *ZSTC* ilifanya zoezi hilo. *(Makofi)*

Hata hivyo, ni lazima nikiri utumiaji wa huduma za benki hasa kwa wananchi wengi waliovijijini bado ni mdogo mno, pamoja na kutumia redio na magazeti katika kuwaelimisha wananchi wetu.

(b) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 71 kwa ajili ya ununuzi wa zao la

karafuu na zaidi ya shilingi bilioni 63 zimekwenda Pemba. Licha ya fedha nyingi kuingia katika Kisiwa cha Pemba, lakini mzunguko wa fedha katika benki zilizoko Pemba umeonekana kuwa ni mdogo mno.

Utafiti uliofanywa Kisiwani Pemba ambao umewajumuisha wakulima 300 umebaini mambo yafuatayo:-

(i) Asilimia 12.9 tu ya wakulima wa Pemba ndio wanaoweka fedha zao benki na asilimia 87.1 hawahifadhi fedha zao benki.
(ii) Uelewa mdogo wa wakulima walio wengi juu ya umuhimu wa kuhifadhi fedha benki.
(iii) Umbali wa upatikanaji wa huduma za kibenki.
(iv) Baadhi ya wakulima kuamua kuwekeza fedha zao nje ya Kisiwa cha Pemba hasa kule Tanzania Bara na hapa Unguja.
(v) Wakulima walio wengi ambao ni wadogo wadogo hutumia fedha hizo katika kukidhi mahitaji yao ya kila siku kama vile kugharamia ujenzi wa nyumba, masomo ya watoto wao na shughuli za matibabu kwa familia zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hizi ndizo sababu za msingi zinazopelekea mzunguko wa fedha usionekane katika benki zilizo Pemba.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika kifungu (b) kwamba utafiti umeshafanyika na kwa mtazamo wa awali, inaoneshwa kuwa upo mzunguko wa fedha katika sekta za ujenzi, biashara, matumizi ya chakula na nguo na ununuzi wa vipando vya usafiri. Kwa taarifa za awali hizo ndio baadhi tu ya sekta ambazo zimeonesha kunufaika zaidi na fedha zilizotokana na karafuu. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, niruhusu nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake fasaha tena ya kina, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa hivi sasa wananchi wengi wa Zanzibar wanaomba waachiwe wapumue, yeye anadhani kwamba tukifikia hatua ya kuachiwa tukapumua, haoni kwamba kuna haja ya wizara yake kuhakikisha inachukua hatua za dhati za kuwaelimisha wananchi wetu umuhimu wa kutumia taasisi kama hizi, ili uchumi wetu ukue na kusaidia kufikia yale malengo ambayo yanayotarajiwa na wananchi baada ya kuachiwa kupumua?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza napokea pongezi zake, pili napokea muono wake kwamba wananchi waendelee kupumua.

Lakini tatu nataka nieleze tu kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na mabenki, tumefanya uamuzi wa makusudi badala ya benki mbili sasa tunataka kuzishirikisha benki zote. Kwa maana hiyo, tunataka kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuhifadhi fedha zao benki. *(Makofi)*

Vile vile tunataka benki zetu zisogeze huduma, ili ziwe karibu zaidi na wananchi na hayo yote tumepanga kuyafanya hasa kwa kuona kwamba mzunguko wa fedha katika mabenki yetu umekuwa mdogo wakati fedha nyingi zimetolewa wakati wa ununuzi wa karafuu. Mhe. Spika, tukifanya hivyo ndio itatusaidia sana fedha hizo kuweza kuonekana katika mabenki yetu. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b)..

(a) Mheshimiwa katika msimu uliopita Serikali ilitumia kiwango hicho cha fedha lakini zaidi Benki ya *PBZ* ilitumia ndege kwa ajili ya kwenda na kurudi kupeleka fedha Pemba. Katika hilo mategemeo ni kwamba fedha zile zikiingia mikononi mwa wakulima zitarudi tena benki ili itengeneze faida kwa njia nyengine. Kwa kuwa hilo halikutokea naomba Mhe. Waziri anieleze ni hasara gani iliyopata *PBZ* kutokana na tatizo hilo.

(b) Lakini vile vile ili kuepuka tatizo hilo kutokea mara ya pili kwa msimu unaokuja, *PBZ* imeandaa mkakati gani kuona kwamba lililotokea mwaka huu lisitokee tena mwaka wa pili. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nimhakikishie katika zoezi la ununuzi wa karafuu *PBZ* haijapata hasara, licha ya kwamba wametumia ndege kwenda Pemba kwa ajili ya kupeleka pesa na kurudi, lakini baadhi ya wakulima na wauzaji wetu wa karafuu waliweka fedha zao benki.

Lakini vile vile *ZSTC* haikuwa na fedha kwa hivyo walilazimika wao kukopa *PBZ* kwa hivyo, *BPZ* kibiashara hii haikupata hasara, ingawa haikupata faida kubwa sana kama ilivyotarajia.

Lakini la pili kwa sababu tumeshaona fedha ipo hasa wakati wa mauzo ya karafuu, *PBZ* ameandaa mikakati kama ifuatavyo:

1. Kama nilivyoeleza zile kambi zote tayari *PBZ* wakishirikiana na *ZSTC* wanazo katika orodha. Hata kabla ya msimu wa karafuu kuanza watafanya zoezi la kupita na kuelimisha wananchi ili msimu utakapoanza tu wananchi wale watakuwa wameshapata taaluma.
2. *PBZ* ataongeza matawi ili awe karibu na wananchi kwa ajili hiyo ya kuweka fedha zao.
3. *PBZ* wakati wa mauzo ya karafuu atakuwa na *mobile bank* ili iweze kuzungumza wananchi wapate fursa ya kuweka fedha zao.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kuwa tatizo moja lililopelekea wananchi wetu kuhifadhi pesa zao mabenki ni kutokana na mabenki kuwa yako mbali na wananchi hao. Je, Mhe. Waziri Wizara yake au serikali ni lini itawarahisishia wananchi hao kuwawekea matawi japo madogo madogo ili waondokane na usumbufu huo na kuhifadhi pesa zao ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kuanzisha matawi madogo madogo ya benki huwezi ukaanzisha kwa msimu wa karafuu, lazima utafiti ufanyike wa kina ibainike kwamba katika eneo hili mzunguko wa pesa upo katika kipindi chote cha miezi 12 ndani ya mwaka. Lakini nataka nimwambie tu Mhe. Kazija kwamba wacha tuliangalie suala hili na tutawaongoza ndugu zetu wa *PBZ* pamoja na mabenki mengine yasogeze huduma zao kama nilivyoeleza awali kwa wananchi ili wananchi wasipate bughudha ya kwenda masafa marefu kufuatilia huduma za benki.

Nam. 64

Ulipaji wa Kodi Vyuo vya Mafunzo

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Chuo cha Mafunzo Zanzibar kimekuwa kikilipa kodi ya shilingi milioni 27 kila mwaka pamoja na kukabiliwa na ufinyu wa bajeti na kusababisha kushindwa kutoa huduma bora za malazi, chakula kwa wafungwa na mahabusu.

(a) Ofisi hii ina mpango gani wa kufuta kodi hiyo ili fedha hizo ziweze kusaidia kuimarisha huduma za Magereza.

(b) Kwa nini Serikali imeamua kutoza fedha hizo wakati bajeti wanayopewa Chuo cha Mafunzo bado haikidhi mahitaji na kulazimika kwa wafungwa na mahabusu kupelekwa kwa miguu hospitali na Mahakamani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali la Mhe. Jaku Hashim Mwakilishi makini wa wananchi wa Jimbo la Muyuni lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa Chuo cha Mafunzo hakilipi kodi Serikalini bali kinakusanya mapato ya Serikali na ni wajibu wao kuyawasilisha mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria za fedha.

(a) Hata hivyo, ofisi yangu haina mpango wa kufuta ukusanyaji wa mapato hayo hadi hapo Serikali itakapoamua vyenginevyo, kwani mapato yanayokusanywa yanatokana na mauzo ya huduma wanazozitoa Chuo cha Mafunzo kwa taasisi na wananchi mbali mbali. Mapato ya Chuo cha Mafunzo yakijumuishwa na yale kutoka taasisi nyengine ndiyo yanayotumiwa na taasisi mbali mbali za Serikali katika kuimarisha huduma za taasisi zetu.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali haitozi kodi kwa Wizara na Taasisi za Serikali, utaratibu ni kwamba taasisi hizo hukusanya mapato yatokanayo na vianzio visivyokuwa vya kodi vinavyosimamiwa na taasisi hizo. Hata hivyo, serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 imechukua hatua ya kuongeza fedha kwenye kasma mbali mbali za Chuo cha Mafunzo ikiwemo kasma ya chakula, ukarabati wa majengo, mafunzo, huduma za wanafunzi na ununuzi wa gari kwa lengo la kusaidia chuo hicho kiweze kutoa huduma bora zaidi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Nashukuru Waziri kakiri kwamba hawakusanyi kodi lakini wanakusanya mapato. Mhe. Spika, kwa kuwa hawakusanyi kodi lakini wanachukua mapato na kwa kuwa mapato haya amekiri kuwa hatayasamehe mpaka pale Serikali itakapoamua. Je, anaonaje katika kipindi hiki cha Mwezi wa Ramadhani sio kama mfute

lakini angalau msamehe kwa kipindi hiki cha Mwezi wa Ramadhani kusudi haya mapato yawasaidie wanafunzi kwa ajili ya kufunga kupata futari na daku inayoridhisha. Mosi.

Pili, kwa kuwa dhamira halisi ya vyuo vyetu vya mafunzo ni kubadilisha mawazo ya uhalifu kuja katika uraia wema na nidhamu nzuri pamoja na kutunza mazingira mazuri yaliyotuzunguka. Kwa sababu mazingira wanayolala wanafunzi ni kupitia virago vya magunia ambavyo vina chawa wengi sana. Je, wanaonaje kama watasamehe angalau kwa kipindi cha mwaka mmoja haya mapato kusudi wakaweza kununuliwa magodoro pamoja na kujengewa vyoo badala ya kutumia mtondoo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kanza nakubaliana na yeye kwamba huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unakaribia na ndugu zetu wale wanahitajia futari nzuri kama sisi tunavyohitajia futari nzuri. *Inshaallah* nasema kwa udhati wa moyo wangu tutahakikisha kwamba wanapata futari nzuri kama sisi wenzao tulioko nje, lakini tusivunje sheria na taratibu za ukusanyaji wa mapato na kuyawasilisha katika Serikali Kuu.

La pili, suala lako nitashirikiana na Mhe. Waziri mwenye dhamana ya Chuo cha Mafunzo, Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili tuweze kuona basi ni kiasi gani hawa ndugu zetu tunaweza kuwapatia magodoro pamoja na kufanya ukarabati vyoo wanavyotumia. Kwa kukudhihirishia hilo Mhe. Mwanamapinduzi katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 Chuo cha Mafunzo tumekipanga kukusanya mapato shilingi 41 milioni. Lakini Serikali itawapa zaidi ya shilingi bilioni sita katika shughuli zao mbali mbali.

Mimi nina imani Mhe. Spika, Waziri mwenye dhamana tutashirikiana kwa karibu zaidi ili fedha iweze kupatikana na kufanya mambo mazuri katika Vyuo vyetu vya Mafunzo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Katika swali la msingi alilouliza Mhe. Jaku moja ameuliza kwamba wafungwa wanapelekwa Hospitali kwa miguu badala ya kuchukuliwa kwa magari. Mhe. Waziri alipojibu swali alisema kwamba watafanya utaratibu wa kuwanunulia gari. Sasa namuuliza Mhe. Waziri kwa sababu vyuo vyetu vya Mafunzo ni vingi viko Unguja na Pemba. Je, katika huo mpango wa kununua magari Mhe. Waziri ana tamaa au amepanga kununua gari ngapi kwa sababu gari moja itakuwa haigawiki na ni muda gani atanunua ilikuondoa tatizo hili lililozungumzwa na Mhe. Jak Hasi

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nilitegemea maswali haya yangetoka wakati wa bajeti ya Ofisi ya Rais lakini Ofisi ya Rais licha ya buti nyingi lakini maswali haya hayakutoka. Hata hivyo, Mhe. Spika, kwa upande wangu mimi kama Waziri mwenye dhamana ya fedha nimetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari, kama fedha zile zitatosha kununulia gari mbili, tatu, nne sisi kibali tumeshawapa wanunue gari. Kwa utaratibu huo Ofisi ya Rais Ikulu kwa kuwa bajeti yao imeshapita wanaweza wakaanza kuomba pesa hizo na wakazipata wakati wowote na wakanunua hizo gari.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa 2012/2013 – Wizara ya Elimu na Matunz o ya Amali

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Bismilahi Rahmani Rahim, Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo ili kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Moh'd Shein kwa umahiri mkubwa wa uongozi katika nyanja zote za maendeleo ya nchi yetu. Mpango aliouanzisha wa kukutana na uongozi wa kila Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kujadiliana nao kuhusu utekelezaji wa malengo ya kazi za wizara hizo kwa kila kipindi cha robo mwaka, umetuwezesha kukutana na yeye mara kwa mara na kufaidika na maelekezo yake, nasaha na muongozo wake katika utekelezaji wa kazi za wizara. Tokea alipoanzisha utaratibu huo umeingia ari ya wafanyakazi wa wizara yangu kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa malengo ya kazi zao.

Mhe. Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa busara, hekima na juhudi zao kubwa za kumshauri na kumsaidia Rais katika kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, aidha napenda niungane na Waheshimiwa Wawakilishi, ndugu, jamaa na marafiki kuwafariji na kuwapa pole wananchi wote wa visiwa vya Unguja na Pemba kutokana na vifo vya wananchi wetu vilivyotokana na kuzama kwa meli ya *M.V. Spice Islanders* siku ya tarehe 10 Septemba 2011. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amin.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwako na Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi wa Jimbo ya Uzini na Bububu Unguja kutokana na vifo vya Waheshimiwa Mussa Khamis Silima na Mhe. Salim Amour Mtondoo waliokuwa Wawakilishi wa majimbo hayo. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao hao mahali pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, vile vile napenda kumpongeza Mhe. Mohammedraza Hassan Dharamsi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi mdogo wa Jimbo hilo uliofanyika tarehe 12/02/ 2012.

Pia, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban ambaye alikuwa Waziri wa Wizara hii kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, na kwa kuweka misingi mizuri alipokuwa Wizarani hapa ambayo sasa inanisaidia.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii vile vile kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa kazi nzuri unayoifanya katika mwaka wa kwanza tangu kuundwa kwa Serikali ya awamu ya saba yenye muundo wa umoja wa kitaifa. Umeonesha uhodari mkubwa katika kusimamia na kuratibu shughuli za Baraza lako tukufu. Pia nampongeza Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza lako tukufu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusaidia wewe.

Mhe. Spika, shukrani zangu pia ziende kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa namna walivyokuwa karibu na mimi katika kuwashajiisha wananchi wa majimbo yao kuendeleza shughuli za elimu Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza lako tukufu ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwa kutuongoza vyema na kutushauri ipasavyo. Wajumbe wa Kamati hii waliweza kuichambua bajeti ya hotuba yangu vizuri sana.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati za moyo wangu kwa msaidizi wangu Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Zahra

Ali Hamadi kwa mashirikiano makubwa anayonipa katika kuyapanga na kuyaendeleza majukumu ya wizara yetu. Aidha, natoa shukrani zangu kwa watendaji na wafanyakazi wote wa wizara yangu wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi na wengine wote kwa mashirikiano mema wanayonipa.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza viongozi wa Baraza la Elimu, Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya, Kamati zote za skuli na wazazi wote kwa michango yao ya hali na mali katika kuziendeleza skuli zetu na hatimae tukafanikiwa kupata maendeleo makubwa ya kielimu katika visiwa vyetu. Pia, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Donge kwa msaada na mashirikiano makubwa wanayonipa hata leo nikafika kuitekeleza kazi hii.

Mhe. Spika, kabla ya kueleza utekelezaji wa mipango ya elimu ya mwaka 2011/2012 na matarajio kwa mwaka 2012/2013, napenda kueleza mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2011/2012.

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, wizara imepata mafanikio yafuatayo:

- Mradi wa kutumia kompyuta kwa ajili ya kufundisha na kufundishia unaoitwa *"21st Century Basic Education"* umezinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein tarehe 28 Februari, 2012.

- Ujenzi wa skuli mpya 13 za sekondari kati ya skuli 16 na Kampasi ya Chuo Kikuu cha Benjamin William Mkapa huko Mchanga Mdogo Pemba umekamilika. Skuli 3 mpya zimefunguliwa na zimeanza kuchukua wanafunzi. Pia ujenzi wa skuli 3 za sekondari za ghorofa katika Mkoa wa Mjini/Magharibi Unguja zinajengwa.

- Ujenzi wa skuli ya msingi inayofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika eneo la Mwanakwerekwe 'C' nao umeanza.

- Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimetimiza miaka kumi tokea kuanzishwa kwake mwaka 2002. Mkuu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar ambae pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameunda kamati

ambayo itachunguza uwezekano wa taasisi nyengine za Elimu ya Juu zilizoko Zanzibar kuweza kuunganishwa na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Kamati hio imeshawasilisha ripoti yake kwa Mkuu wa Chuo na hivi sasa inaandaa utaratibu wa taasisi nyengine za Elimu ya Juu zilizoko Zanzibar kuweza kuunganishwa na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

- Chuo cha Kiislamu cha Mazizini kimesherehekea miaka 40 tokea kuanzishwa kwake. Mkakati unaandaliwa chuo hiki kiwe au halafu kidogo kiwe ni Chuo Kikuu kikamilifu.

- Jumla ya vijana 1,086 wamedhaminiwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar katika kipindi cha 2011/2012.

- Asilimia ya uandikishaji wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi imeongezeka kutoka 118.5 mwaka 2011 hadi 121.5 mwaka 2012. Pia uandikishaji katika ngazi ya elimu ya sekondari imeongezeka kutoka 67.2 mwaka 2011 hadi 68.0 mwaka 2012. Katika ngazi zote hizo asilimia ya uandikishaji kwa wasichana imekuwa kubwa zaidi kuliko ya wavulana.

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho yametokana na uongozi mzuri na wa busara wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na ufuatiliaji wake wa karibu wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hali hiyo imetuwezesha kutekeleza kwa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 ya Chama cha Mapinduzi na Sera na Mikakati madhubuti ya Chama hicho. Aidha, kuendelea kuwepo kwa amani, utulivu na mshikamano wa wananchi wote kupitia Serikali yao ya Mapinduzi yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa kumechangia sana kuleta mafanikio yaliyopatikana.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa wananchi wote wa Zanzibar kwa michango yao ya hali na mali katika kuendeleza sekta ya elimu na mafunzo ya amali. Aidha, nawashukuru viongozi katika ngazi mbali mbali, wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuwahamasisha na kuwasaidia wananchi wa majimbo yao kuiendeleza sekta hii ya elimu. Vile vile nawashukuru Washirika wetu wa maendeleo kwa kutuunga mkono katika juhudi zetu hizi za maendeleo. Miongoni mwa washirika hao ni Jamhuri ya Watu wa China, India, Mashirika ya Kimataifa ya *Sida*, *USAID*, *UNICEF*, *UNESCO* na "*Book Aid International*". Pia tunazishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*),

Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*Badea*) na Benki ya Dunia. Aidha, nawashukuru washirika wenzetu kama vile *TASAF*, *FAWE* - Zanzibar, "*Save the Children*" na *ZAYADESA* kwa misaada yao mikubwa.

Mhe. Spika, baada ya kuelezea kuhusu malengo ya bajeti ya wizara kwa mwaka 2011/2012, kwa heshima naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa shughuli zetu za maendeleo za idara moja moja na taasisi zinazojitegemea kwa mwaka 2011/2012 na matarajio na malengo kwa mwaka 2012/2013.

IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti ina majukumu ya kuandaa mpango wa mwaka na mpango mkakati wa maendeleo wa muda wa kati wa Wizara, kuratibu na kufuatilia rasilimali na misaada mbali mbali ya wahisani kwa kazi za maendeleo za Wizara, kusimamia, kufanya mapitio ya tathmini ya sera, mpango, programu na miradi ya Wizara, kuratibu ufuatiliaji na tathmini wa shughuli zote za kielimu pamoja na miradi ya Wizara, kuratibu maandalizi, mapitio na ufuatiliaji wa sera mbali mbali za elimu, kuratibu shughuli za utafiti wa kielimu na kutayarisha maelezo ya kisera kutokana na tafiti hizo na kusimamia ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa takwimu mbali mbali za Wizara.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 wizara ilipanga kutekeleza jumla ya miradi tisa ya maendeleo. Miradi hiyo imetekelezwa kwa pamoja baina ya serikali, wananchi na washirika wa maendeleo. Miradi hiyo ilitengewa jumla ya shilingi 57,310,054,000/= ambapo kati ya hizo shilingi 4,500,000,000/= ni mchango wa SMZ; shilingi 4,000,000,000/= ni ruzuku kutoka *Sida*, *UNICEF* na *UNESCO*, shilingi 8,310,054,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika na shilingi 40,500,000,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 3,615,000,000/= za SMZ zilitolewa ikiwa ni sawa na asilimia 80.3 ya makadirio. Kwa upande wa washirika wa maendeleo, fedha zilizopatikana ni Tsh. 21,585,548,444/= sawa na asilimia 45.9 ya makadirio.

Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maktaba

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya Tsh. 200,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa tawi la Maktaba Kuu Pemba. Hadi kufikia

tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 155,000,000/= sawa na asilimia 77.5 ya fedha zote zimepatikana. Sehemu ya fedha hizo zimetumika kwa matayarisho ya ujenzi husika ikiwemo kuandaa michoro na "Bills of quantities".

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 200,000,000/= za SMZ na Tsh. 419,200,000/= za UNICEF. Malengo ya mradi huu yalikuwa ni:-

(i) Kuendelea kutoa mafunzo ya mtaala mpya kwa walimu wa elimu ya maandalizi.

(ii) Kuanza kutoa mafunzo ya walimu wa maandalizi 1,000 kwa njia ya redio.

(iii) Kununua vifaa vya kufundishia.

(iv) Kutayarisha sera ya elimu ya maandalizi.

(v) Kuendelea na ujenzi wa skuli za maandalizi

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 110,000,000/= sawa na asilimia 55 ya fedha zote za SMZ zimetolewa na kutumika. Kwa upande wa UNICEF, Tsh. 51,264,700/- sawa na asilimia 11 zimepatikana na utekelezaji halisi ulikuwa kama ifuatavyo:-

i) Warsha ya Makatibu Wakuu wa Wizara Nne zikiwemo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na wajumbe wa Kamati ya "ECD Resource Pack." ilifanyika kwa madhumuni ya kuandaa kwa pamoja Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (*Intergrated Early Childhood Care and Development Policy*).

ii) Jumla ya seti 180 za meza na viti vya walimu na wanafunzi wa skuli ya maandalizi Potoa zimechongwa. Pia jumla ya meza 80 na viti 160 vya walimu na wanafunzi wa skuli ya maandalizi Ungi – Msuka vimechongwa.

iii) Ujenzi wa skuli ya maandalizi Tunduni umekamilika kwa hatua ya kuezeka, plasta, sakafu, aproni na rangi.

iv) Mihutasari ya elimu ya maandalizi imepitiwa na kurekebishwa. Pia, mafunzo ya walimu juu ya matumizi ya mihutasari mipya yatatolewa baada ya kuchapishwa mihutasari iliyorekebishwa.

v) Moduli ya kwanza na ya pili za kutolea mafunzo ya walimu wa maandalizi kwa njia ya redio zimeandikwa. Mafunzo kwa walimu yatatolewa baada ya kukamilisha uandishi wa moduli nyengine nne.

Mradi wa Uimarishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar

Mhe. Spika**,** mradi huu unatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (Badea) na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa majengo manne ya chuo
(ii) Kununua samani, vifaa vya maabara na vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
(iii) Kuanza kutumia majengo.

Mradi ulipangiwa jumla ya Tsh. 1,725,000,000/= za SMZ na Tsh. 4,380,000,000/= za Badea. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012 jumla ya Tsh. 1,610,000,000/= za SMZ sawa na asilimia 93.3 ya makadirio zilipatikana. Aidha, kwa upande wa Badea, Tsh. 759,737,056/= zilipatikana sawa na asilimia 17.3 ya makadirio. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa majengo manne ya chuo unaendelea. Kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 90.

(ii) Wizara imetiliana saini na wazabuni wa vifaa na kemikali za maabara za Fizikia, Kemia na Biolojia. Vifaa vya Fizikia tayari vimepokelewa.

(iii) Baadhi ya samani zimeanza kupokelewa

(iv) Mzabuni wa kuleta vifaa vya kompyuta amechaguliwa na Wizara itatiliana nae saini mkataba hivi karibuni.

(v)

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi

Mhe. Spika**,** mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya wananchi, SMZ, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Sida USAID na UNICEF. Mradi ulitengewa jumla ya Tsh. 1,000,000,000/= za SMZ na Tsh. 4,969,938,000/= kutoka Sida na UNICEF na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 200 kwa kushirikiana na wananchi.

(ii) Kufanya ukarabati wa skuli 15 za msingi.

(iii) Kuchonga madawati 5,000 ya wanafunzi wa skuli za msingi.

(iv) Kukamilisha ujenzi wa nyumba tatu za walimu.

(v) Kujenga skuli moja ya msingi katika Wilaya ya Magharibi.

(vi) Kuandika na kuchapisha moduli za kutolea mafunzo kazini kwa walimu wa Sayansi na Hisabati wa madarsa ya tano na sita.

(vii) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa "21st Century Basic Education."

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 1,000,000,000/= za SMZ zilipatikana sawa na asilimia 100 ya makadirio. Kwa upande wa Sida na UNICEF fedha zilizotolewa ni Tsh.359,576,800/- sawa na asilimia 8 ya makadirio. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa madarasa mapya 116, kumbi za mitihani 02, ofisi 28, vyumba vya kompyuta 01, na ghala 04 umekamilika.

ii) Ukarabati wa majengo wa skuli za Donge msingi, Fujoni, Mkunazini, Mwembemakumbi, Kidongo-chekundu, na Kiboje kwa upande wa Unguja na Piki, Minungwini, Shumba, Michenzani na Mitiulaya kwa upande wa Pemba umefanyika.

iii) Jumla ya madawati 1,560, viti 124 na meza 124 yamechongwa na kusambazwa katika madarasa 120

ya skuli za msingi yaliyojengwa kwa msaada wa shirika la Misaada la Sweden (Sida) katika bajeti ya mwaka wa fedha 2010/2011. Aidha jumla ya madawati mengine 173 yamechongwa kwa fedha za SMZ na kusambazwa katika skuli za Unguja (90) na Pemba (83).

iv) Wizara imetiliana saini mkataba wa ujenzi wa skuli ya msingi na kampuni ya *"Fujian Construction Engineering group*" ya China katika eneo la Mwanakwerekwe. Kazi za ujenzi zimeanza.

v) Rasimu za awali ya miongozo kuhusu maji, afya na mazingira kwa ajili ya skuli zetu zimeandikwa na kuchapishwa. Kazi ya uhariri inaendelea.

vi) Kazi ya uandishi wa moduli ya somo la Sayansi inaendelea na taratibu za kumpata mshauri mwelekezi ataeongoza kazi ya uandishi na uchapaji wa moduli za kutolea mafunzo kazini kwa walimu wa Hisabati zimeanza.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya SMZ, Benki ya Dunia na Badea. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mradi huu ulikuwa na malengo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa skuli mpya 16 za sekondari Unguja na Pemba.

(ii) Kuchonga seti 20,750 za meza na viti kwa ajili ya wanafunzi wa skuli za sekondari.

(iii) Kununua vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa skuli za sekondari.

(iv) Kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa cha Mchangamdogo.

(v) Kuendelea na ukarabati wa skuli za sekondari za Forodhani, Tumekuja, Hamamni, Fidel-castro, Utaani na Uweleni.

(vi) Kuanza ujenzi wa skuli mpya za sekondari za ghorofa katika maeneo ya Kiembe-samaki, Mpendae, Kwamtipura, Kibuteni na Mkanyageni.

(vii) Kuandika, kuchapisha na kusambaza vitabu vya kiada na miongozo ya walimu wa madarasa ya I – IV.

Mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 850,000,000/= za SMZ, Tsh. 40,500,000,000/= za Benki ya Dunia na Tsh. 3,930,054,000/= za Badea. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 407,000,000/= za SMZ sawa na asilimia 47.9 ya makadirio zilipatikana. Aidha Tsh. 20,235,644,508/= za Benki ya Dunia sawa na asilimia 50 zilipatikana. Pia Tsh. 144,864,350/= za Badea sawa na asilimia 17 zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa skuli 13 za sekondari kati ya 16 umekamilika na hatua za makabidhiano na uchukuaji wa wanafunzi zinaendelea. Ujenzi wa skuli za sekondari za Tunguu, Paje-mtule na Dimani umefikia asilimia 70 ya ukamilishwaji wake.

ii) Jumla ya seti 3,470 za meza na 4,562 za viti vya wanafunzi na walimu zimechongwa na kusambazwa katika skuli mpya za sekondari za Shamiani, Matemwe, Chaani, Mwanda, Dole, Uzini na Chuo cha Ualimu Benjamin Mkapa Kampasi ya Mchangamdogo. Uchongaji wa samani kwa ajili ya skuli nyengine mpya za sekondari unaendelea. Pia, Wizara kwa kutumia fedha za SMZ imechonga meza na viti 500 vya wanafunzi na kusambazwa katika skuli za sekondari za Fuoni, Pale na Mtende.

iii) Jumla ya vitabu 190,212 vya masomo ya Kiswahili (65,000), Historia (56,000) Jiografia (56,000), Kompyuta (12,700) na Mafunzo ya Ualimu (512) vimenunuliwa. Baadhi ya vitabu hivi vimegawiwa

katika skuli za sekondari zilizopo. Ugawaji wa vitabu hivyo kwa skuli mpya za sekondari utafanyika baada ya ujenzi wake kukamilika na kukabidhiwa kwa Wizara.

iv) Awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la madarasa na Uongozi la Chuo cha Ualimu Benjamin William Mkapa eneo la Mchanga-mdogo umekamilika na kukabidhiwa Wizara. Ujenzi wa nyumba za walimu na dakhalia unaendelea.

v) Ukarabati wa skuli za sekondari za Fidel -Castro, Utaani, Tumekuja na Forodhani unaendelea. Pia, ukarabati wa skuli za sekondari za Hamamni na Uweleni umeanza.

vi) Ujenzi wa skuli mpya za sekondari za ghorofa katika maeneo ya Kiembe- samaki, Kwamtipura na Mpendae umeanza. Pia, wakandarasi wa ujenzi wa skuli za sekondari za ghorofa za Kibuteni na Mkanyageni wamechaguliwa na Wizara itatiliana saini mkataba hivi karibuni.

vii) Ujenzi wa madarasa mapya katika skuli za sekondari za Miwaleni, Mfenesini na Potoa unaendelea. Ukarabati wa majengo ya skuli ya sekondari ya Benbella (ufa) na sekondari Kengeja (jengo la madarasa matatu) umekamilika.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mradi ulipangiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya ushirika vya wanawake na kwa wahitimu kutoka vituo vya amali ili waweze kujiajiri na kuendeleza fani walizosomea.

(ii) Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Mtemani

(iii) Kuanza utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa Elimu Mbadala na Amali

Jumla ya Tsh. 100,000,000/= za SMZ zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012 jumla ya Tsh. 100,000,000/= za SMZ zimepatikana sawa na asilimia 100 ya makadirio. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i) Maombi ya mikopo kutoka vikundi 20 vya ushirika yamepokelewa. Hata hivyo, hakuna mikopo mipya iliyotolewa kutokana na kuwepo kwa madeni makubwa ya kipindi cha nyuma. Zoezi la kukusanya madeni kutoka kwa vikundi vilivyokopeshwa hapo awali lilifanyika. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 kati ya deni lote la Tsh. 749,433,000/=, Tsh. 491,875,000/= sawa na asilimia 65.6 la deni lote zilikusanywa. Fedha ambazo bado zinadaiwa ni Tsh. 257,558,000/=.

ii) Kazi za ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala Wingwi Mtemani zimefikia hatua ya kupiga plasta ya ndani na nje.

iii) Awamu ya pili ya mradi wa Elimu Mbadala na Amali unatarajiwa kuanza hivi karibuni baada ya Serikali kutimiza masharti yote na mradi unatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni. Mpango kazi wa utekelezaji wake wa miezi 15 ya mwanzo umetayarishwa na kuwasilishwa AfDB kwa kupatiwa fedha.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi

Mhe. Spika, mradi huu umetekelezwa na SMZ pekee na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa madarasa manne mapya katika skuli ya sekondari ya ufundi Kengeja.
(ii) Kuipatia skuli ya sekondari ya ufundi Kengeja vifaa vya karakana
(iii) Kuendelea na ukarabati wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Jumla ya Tsh. 400,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya kukamilisha malengo yaliyowekwa. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 158,000,000/= zimepatikana ikiwa ni sawa na asilimia 39.5 ya makadirio. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa madarasa manne mapya ya skuli ya sekondari ya ufundi Kengeja umekamilika.

ii) Zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya karakana ya umeme vya skuli ya Kengeja ufundi zimefanyiwa tathmini. Taratibu za kutiliana saini mkataba wa ununuzi wa vifaa husika na mzabuni aliyeshinda zinaendelea.

iii) Vitabu na vifaa nyengine vya kufundishia katika Taasisi ya Karume ya sayansi na teknolojia vimenunuliwa, ukarabati wa vyoo vya jengo la ICT na milango ya "workshop" umefanyika na ukarabati wa dakhalia ya wasichana na wavulana umekamilika.

Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Kiislamu Micheweni

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa na SMZ pekee na ulikuwa na malengo yafuatayo:-

i. Kujenga uzio kuzunguka eneo la chuo
ii. Kuendeleza ukarabati wa majengo yaliyopo.

Mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 50,000,000/=. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 50,000,000/= sawa na asilimia 100 ya makadirio zilipatikana. Sehemu ya fedha hizo zimetumika kwa kufyatua matofali 10,000/- na kununua vifaa vyengine kwa ajili ya ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la chuo. Ujenzi wa uzio haukuunza.

Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 25,000,000/= kutoka SMZ pekee na ulikuwa na lengo la kutayarisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la pili la Wizara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2012, jumla ya Tsh. 25,000,000/= sawa na asilimia 100 ya makadirio zimepatikana. Michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la pili la Wizara imeandaliwa. Pia, baadhi ya ofisi za jengo liliopo zimefanyiwa ukarabati.

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inatarajia kutekeleza miradi kumi ya maendeleo. Kati ya hiyo, miradi minne itatekelezwa kutokana na bajeti ya SMZ pekee na miradi sita itatekelezwa kwa pamoja baina ya serikali na washirika wa maendeleo wa ndani na nje. Jumla ya Tsh. 5,100,000,000/= za SMZ na Tsh. 3,208,315,000/= ambazo ni ruzuku kutoka kwa washirika mbali mbali wa maendeleo na Tsh. 30,660,976,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (Badea) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Malengo ya miradi ni kama ifuatavyo:-

Mradi wa Upanuzi na Uimarishaji wa Huduma za Maktaba

Mhe. Spika, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee na utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa tawi la maktaba kuu Pemba.
ii) Kujenga msingi wa jengo jipya.
iii) Kufanya ukarabati wa jengo la maktaba liliopo.

Mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 200,000,000/= za SMZ.

Mradi wa Uimarishaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Mhe. Spika, mradi huu utatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (Badea) na utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kufunga vifaa vya ICT na vipoza hewa katika majengo mawili.
ii) Kuweka miundombinu kwa ajili ya mawasiliano ya simu na “internet”.
iii) Kununua vifaa vya kufundishia kwa ajili ya Kitivo cha Uhandisi.
iv) Kukamilisha kazi za ujenzi na kusambaza miundo mbinu ya umeme.
v) Kuanza kutumiwa kwa majengo

Mradi huu umepangiwa Tsh. 1,725,000,000/= za SMZ na Tsh. 4,332,959,000/= kutoka Badea.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi

Mhe. Spika, mradi huu utatekelezwa kwa mashirikiano kati ya wananchi, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na mashirika mbali mbali ya maendeleo yakiwemo Sida, UNICEF, UNESCO na USAID. Mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 150 kwa kushirikiana na wananchi katika Wilaya tisa za Unguja na Pemba.
ii) Kufanya ukarabati katika skuli 15 za msingi.
iii) Kuchonga madawati 2,250 na kuyasambaza katika madarasa mapya yatayojengwa.
iv) Kuwapatia walimu mafunzo mbali mbali yakiwemo ya matumizi ya lugha ya Kiingereza kwa ajili ya kufundishia, mafunzo juu ya matumizi ya mtaala mpya wa ngazi ya msingi na mafunzo juu ya kufundisha katika mfumo wa elimu mjumuisho.
v) Kukamilisha ujenzi wa nyumba tatu za walimu.
vi) Kuendeleza ujenzi wa skuli moja ya msingi katika eneo la Mwanakwerekwe.
vii) Kutoa mafunzo kwa walimu na kamati za skuli juu ya kuimarisha huduma za maji, afya na mazingira katika skuli.
viii) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Tz – 21.

Mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 800,000,000/= za SMZ, Tsh. 2,937,061,000/= kutoka Sida na Tsh. 108,000,000/= kutoka UNICEF.

Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Kiislamu

Mhe. Spika, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee na utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kujenga uzio kuzunguuka eneo la Chuo cha Kiislamu Micheweni na Chuo cha Kiislamu Mazizini
ii) Kuendeleza ukarabati wa majengo ya Chuo cha Kiislamu Micheweni yaliyopo.

Jumla ya Tsh. 25,000,000/= za SMZ zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha malengo hayo.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali

Mhe. Spika, hii ni awamu ya pili ya mradi huu ambao utatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika.(AfDB). Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, mradi utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya ushirika 20 vya wanawake wajasiriamali na kwa wahitimu kutoka vituo vya mafunzo ya amali.

ii) Kuendeleza ujenzi wa kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Mtemani Pemba.

iii) Kutafuta washauri elekezi na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya elimu mbadala vitatu, vituo vya mafunzo ya amali viwili, upanuzi na ukarabati wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, upanuzi na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar na ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.

iv) Kuandaa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wakufunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar na wakufunzi wa Mafunzo ya amali

v) Kupitia na kurekebisha mitaala ya mafunzo kwa wanafunzi wa vituo vya Elimu Mbadala

vi) Kununua vifaa na magari kwa ajili ya Ofisi ya Uratibu wa Mradi na Kamisheni ya Kazi.

Jumla ya Tsh. 100,000,000/= za SMZ na TSh. 1,994,098,000/= za AfDB zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali, Benki ya Dunia na Badea. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 mradi huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

i) Kukamilisha ujenzi wa skuli za sekondari za ghorofa za Kiembesamaki, Kwamtipura na Mpendae.

ii) Kukamilisha ujenzi wa skuli za Sekondari za Miwaleni, Donge, Maungani, Makongeni na Chanjamjawiri zilizoanzishwa na wananchi.

iii) Kukamilisha ujenzi wa skuli mpya za Sekondari za Paje mtule, Tunguu na Dimani.

iv) Kukamilisha ukarabati wa skuli za sekondari za Tumekuja, Fidel Castro, Forodhani, Uweleni, Hamamni na Utaani.

v) Kuchonga seti 2,000 za meza na viti kwa madarasa ya sekondari yaliyomalizika kujengwa.

vi) Kuanza ujenzi wa skuli mpya za sekondari za Kibuteni Unguja na Mkanyageni Pemba.

vii) Kuandika, kuchapisha na kusambaza vitabu vya kiada na miongozo ya walimu wa madarasa ya I – IV.

viii) Kuandika na kuchapisha moduli za kutolea mafunzo kazini kwa walimu wa Sayansi na Hisabati wa msingi.

ix) Kutoa mafunzo kwa walimu wa msingi na sekondari.

x) Kutoa mafunzo kwa walimu wakuu juu ya uendeshaji wa skuli.

Mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 900,000,000/= za SMZ, Tsh. 24,000,000,000/= za Benki ya Dunia na Tsh. 3,930,054,000/= za Badea.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, mradi huu utatekelezwa na SMZ pekee. Malengo ya mradi huu ni kama ifuatavyo:-

i) Kuanza ujenzi wa dakhalia mpya ya skuli ya sekondari ya Ufundi Kengeja.

ii) Kuipatia skuli ya sekondari ya Ufundi Kengeja vifaa vya karakana.

iii) Kuendelea na ukarabati wa majengo, kununua vifaa vya kufundishia na vitabu kwa ajili ya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 400,000,000/= za SMZ kwa ajili ya kukamilisha malengo yaliyopangwa.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, mradi huu utatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na UNICEF. Malengo ya mradi huu ni kama ifuatavyo:-

i) Kuendelea kutoa mafunzo ya mtaala mpya kwa walimu wa elimu ya maandalizi.
ii) Kuandika na kuchapisha moduli kwa ajili ya walimu wa maandalizi kwa njia ya redio.
iii) Kuanza kutoa mafunzo ya walimu wa maandalizi 1,000 kwa njia ya redio.
iv) Kununua vifaa vya kufundishia
v) Kujenga na kuchonga samani za skuli mbili mpya za maandalizi.
vi) Kununua vifaa vya kufundishia.

Mradi huu umetengewa jumla ya Tsh. 200,000,000/= za SMZ na Tsh. 491,200,000/= za UNICEF.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi kwa Wilaya ya Magharibi:

Mhe. Spika**,** mradi huu ni mpya na una madhumuni ya kuimarisha utoaji wa elimu ya msingi kwa skuli za Wilaya ya Magharibi kwa kuongeza madarasa kwa lengo la kupunguza wingi wa wanafunzi madarasani. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itakamilisha ujenzi wa madarasa 70 yaliyoanzishwa na wananchi na kuchonga madawati 1,050. Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 800,000,000/= za SMZ.

Mradi wa Sayansi na Teknolojia:

Mhe. Spika**,** mradi huu unatekelezwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa mashirikiano na Benki ya Dunia.

Mradi huu una malengo yafuatayo:-

(i) Kununua vifaa vya maabara za sayansi na ICT.
(ii) Kusomesha wakufunzi katika ngazi ya shahada ya pili na ya tatu.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, mradi umepangiwa kutumia Tsh. 830,529,600/= za Benki ya Dunia.

Utafiti

Mhe. Spika, shughuli za utafiti zimeendelea kufanyika katika kipindi hiki. Wizara imekamilisha uandishi wa ripoti ya utafiti mkuu wa SACMEQ III na kuiwasilisha "International Institute for Educational Planning (IIEP)" Paris. Matokeo ya awali ya utafiti mkuu wa SACMEQ III, utafiti wa elimu bila ya malipo na utafiti juu ya "*School Effectiveness and Self Evaluation at Central*

System and School levels" yaliwasilishwa na kujadiliwa kwa walimu wakuu wa skuli za msingi na sekondari za Unguja na Pemba pamoja na wadau wengine na sekta ya elimu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imekusudia kuendelea kuwasilisha matokeo ya utafiti mkuu wa SACMEQ III kwa walimu hasa wanaosomesha madarasa ya sita. Wizara itaendelea na matayarisho ya utafiti mkuu wa SACMEQ IV unaotarajiwa kufanyika mwezi Septemba 2013. Pia Wizara kwa kushirikiana na Shirika la UNESCO itafanya tathmini kuhusu mafanikio na changamoto za Elimu kwa Wote kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita "EFA- End of Decade Assessment". Pia, Wizara kwa kushirikiana na UNESCO itaendesha zoezi la utafiti kuhusu hali ya kisomo cha elimu ya Watu Wazima (*Literacy survey*).

Ukusanyaji na Uchambuzi wa Taarifa za Elimu

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la USAID iliendelea na kazi ya kuimarisha ukusanyaji wa takwimu mbali mbali za elimu kwa kutoa mafunzo kwa watendaji. Mafunzo yametolewa kwa watendaji wa divisheni ya EMIS juu ya uchambuzi na ukusanyaji wa takwimu ya programu maalumu itakayochambua takwimu za skuli (school database). Mafunzo hayo yaliendeshwa na kampuni ya "A*gile Learning* "ya Marekani.

2. Katika mwaka 2012/2013 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Marekani USAID, inaandaa programu maalum (*Database*) kwa ajili ya kuweka na kuchambua taarifa za elimu za Zanzibar. Programu hii itatumika katika ngazi ya skuli, Wilaya na Wizarani. Programu ya skuli itakuwa na uwezo wa kuweka taarifa za mwanafunzi mmoja mmoja ili kuweza kutathmini maendeleo yao ya elimu. Pia, kila skuli itapatiwa kompyuta mbili kwa ajili ya kukusanya na kuhifadhi takwimu. Pia, mafunzo ya matumizi ya kompyuta hizo na uwekaji wa kumbukumbu yatatolewa kwa walimu watakwimu wa skuli ili waweze kutumia programu hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Maendeleo ya Kisera

Mhe.Spika**,** Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imefanya tathmini ya Mpango wa miaka mitatu ya utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Elimu Zanzibar (ZEDP). Tathmini hiyo imeonesha kwamba hatukufanikiwa kutekeleza baadhi ya malengo ya mpango wetu wa miaka mitatu kutokana na ufinyu wa bajeti yetu na kukosekana kwa misaada ya kutosha kutoka kwa wahisani wetu.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakusudia kuandaa awamu ya pili ya Mpango wa miaka mitatu wa utekelezaji wa Mpango Mkuu

wa Maendeleo ya Elimu Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 hadi 2015/2016 sambamba na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini wa Zanzibar wa mwaka 2010.

Ufuatiliaji na Tathmini.

Mhe. Spika**,** Wizara, imefanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa malengo yaliyojipangia. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kwa ushirikiano na UNESCO iliandaa mafunzo ya muda mfupi kwa baadhi ya maafisa wake juu ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na kuandaa mpango wa kuwajengea uwezo maafisa wote wanaoshughulika na ufuatiliaji na tathmini. Pia tathmini ilifanyika ya Mradi wa Elimu ya lazima unaogharimiwa kwa pamoja na Benki ya Dunia. Tathmini hio ilionesha mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mradi huo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakusudia kuendelea kutoa mafunzo juu ya ufuatiliaji na tathmini kwa maafisa wake waliobakia kufuatana na mpango uliotayarishwa. Aidha Idara, itaendeleza kazi za ufuatiliaji na tathmini ya mpango ya kazi mbali mbali ya Wizara na kutoa ripoti za tathmini hiyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 1,444,000,000/- kwa Unguja na Tsh 172,000,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika**,** Idara hii ina majukumu ya kusimamia masuala yote ya kiuendeshaji na ya wafanyakazi wote yakiwemo maswala yanayohusiana na utumishi, utunzaji wa kumbukumbu za wafanyakazi, uendelezaji wa wafanyakazi kitaaluma na mafunzo na kuwapatia huduma nyenginezo zitakazosaidia kuwaongeza ari ya kufanya kazi na kuleta ufanisi zaidi. Pia, Idara inaratibu matumizi na utunzaji wa majengo yote ya Wizara na Taasisi zake.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 13,675 kati yao wanawake ni 8,379 na wanaume ni 5,296. Wafanyakazi 9,995 wapo Unguja na 3,680 wapo Pemba. Kati ya wafanyakazi wote, wafanyakazi 12,592 wako katika kada ya uwalimu. Pia, jumla ya walimu 195 waliajiriwa, kati yao 02 wa shahada ya uzamili, 137 shahada ya kwanza, (43 wa sayansi na 94 wa sanaa), 55 wa stashahada (53 wa sayansi na 02 sanaa) na 01 cheti cha ualimu. Wizara inatarajia kupata walimu wa kujitolea 15 wa masomo ya sayansi na Hisabati kutoka Nigeria.

Mhe. Spika**,** Wizara inathamini juhudi za wafanyakazi wake kujiendeleza. Jumla ya wafanyakazi 575 wameruhusiwa kujiunga na masomo ya ngazi mbali mbali, kati yao wafanyakazi 05 wanachukua mafunzo ya cheti, 253 mafunzo ya stashahada, 270 mafunzo ya shahada ya kwanza, wafanyakazi 45 mafunzo ya shahada ya uzamili na wafanyakazi 02 shahada ya uzamivu. Pia jumla ya wafanyakazi 32 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika nchi za China na India. Wizara inazishukuru na kuzipongeza, Ofisi za Ubalozi Mdogo wa India na China kwa kuwapatia watendaji wetu nafasi za mafunzo katika nchi zao.

Mhe. Spika**,** katika mwaka 2011/2012, wafanyakazi 95 walistaafu kazi kwa mujibu wa sheria, 28 walifariki dunia (Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amini), 02 walifukuzwa kazi kwa makosa mbali mbali na 07 waliacha kazi kwa hiari yao. Aidha wafanyakazi 17 walipewa uhamisho kwenda kuendelea na kazi katika taasisi mbalimbali za Serikali na wengine 57 walichukua likizo bila ya malipo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ilinunua vyombo vya usafiri na vitendea kazi mbali mbali ambavyo vimesaidia sana katika kuinua ufanisi wa kazi. Wizara ilinunua gari moja kwa matumizi ya mradi wa ujenzi wa skuli mbili za sekondari. Pia vespa 13 zilinunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Idara mbali mbali zikiwemo vespa 2 kwa ajili ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Ofisi ya Michezo Unguja (1), Idara ya Elimu Maandalizi na Msingi (1), Idara ya Ukaguzi wa Elimu - Pemba (2), Idara ya Elimu Mbadala na Watu wa Wazima (1), Kitengo cha Uhasibu (1), Kitengo cha Ununuzi wa Ugavi (1) na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali (4). Vyombo hivyo vya usafiri vimewarahisishia wafanyakazi wetu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Idara pia iliwadhamini wafanyakazi 1,029 (845 Unguja na 184 Pemba) walioomba mikopo ya fedha, vipando na vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kujiendeleza kimaisha. Mikopo hiyo imetolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya Posta na Elimu SACCOS.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara inakusudia kuandaa mpango wa mafunzo wa Wizara, kukamilisha upembuzi yakinifu wa mahitaji wa walimu kwa kila skuli na kwa kila somo, kuwapatia mafunzo maalum maofisa wa Uendeshaji na Utumishi wa Idara na Taasisi za Wizara, kuandaa mpango wa rasilimali watu, kuendelea kuwapatia vitendea kazi wafanyakazi na kuwapatia huduma ya likizo wafanyakazi kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu. Aidha Wizara itaendelea kuajiri wafanyakazi wa kada mbali mbali kulingana na mahitaji yanayojitokeza.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, inaonesha Mhe. Waziri hotuba yake haiandani sambamba na vitabu tulivyopewa sisi. Sasa nilikuwa naomba aidha Mhe. Waziri aidha akisome hiki kitabu tulichopewa sisi ili twende sambamba au huu muhutasari wake, kwa sababu kila tunavyofuatilia yeye na sisi tunaona hatwendi sambamba, sasa tunaweza tukaja kumuuliza maswali Mhe. Waziri ambayo pengine kwenye kitabu hayamo. Sasa nilikuwa naomba kidogo tupate ufafanuzi wa ziada.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri sijui kama unakusudia kusoma sehemu fulani halafu unatu-refer kwenye page fulani ili sasa uelekee page nyengine kwa sababu utaratibu huo wa kufupisha huwa tunautumia lakini huwa unatueleza tu, umeeleza sehemu fulani halafu unatu-refer kwa maelezo zaidi aangalia page moja, mbili tatu, kitu kama hicho au sijui kama tofauti gani, labda ungetupatia maelezo kidogo ili tukaweza kuendelea au vyengnevyo itakuwa ni tatizo basi tuchukue ushauri wa Mhe. Hamza.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ninachokisoma ni bajeti yangu katika kitabu na huu ni muhutasari. Kwa sababu wizara yangu ni kubwa sana, bajeti yake ina kurasa 110, si rahisi kuzisoma kurasa hizo kwa kipindi hiki na ndio maana kama wanavyofanya wengine, nimetengeneza muhutasari wa bajeti na ukiisoma ukiisikiliza vizuri bajeti yangu ninapoisoma na hatimaye ukirudi katika kitabu utakuta yote niliyoyasoma yamo katika kitabu, ukitaka kuchangia haya ninayosoma ni sawa, ukitaka kuchangia kwenye kitabu ni sawa.

Mimi nipo tayari kusikiliza michango yote itakayotolewa ama kwa muhutasari au kwa kupitia kwenye kitabu.

Mhe. Spika: Ni utaratibu ambao tuliokuwa tumejiwekea kwamba kama hotuba ya Mhe. Waziri ni refu ya kutosha, tunao utaratibu wa kuweza kuandika kwa kifupi ilimuradi tu pale Mhe. Waziri anaposoma anasoma maeneo fulani ambayo anataka kuya-highlight masuala muhimu, lakini kwa maelezo mengine ya ziada huwa Mhe. Waziri anatuelekeza Waheshimiwa Wajumbe tuangalie katika maeneo ya ukurasa fulani hadi ukurasa fulani. Kama hivyo ndivyo ambavyo umefanya Mhe. Waziri ruhsa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ndivyo nilivyofanya kwenye takwimu na maelezo ya ziada.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, ninadhani utaratibu wetu mara nyingi unakuwa hata mtu anapokuja kuzuia kifungu, atakiwa mtu anapokuja kuzuia kifungu azuiwe kwa kile ambacho Mhe. Waziri alichokisema.

Sasa anaposema vyengine na kitabu kinasema vyengine na ndio maana nikashauri ni vizuri bora Mhe. Waziri akakisoma hiki kitabu chenyewe, kwa sababu kwa mfano mimi katika kitabu ukurasa wa 8 hiki nilichokuwa nacho mimi, ukija katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa mwaka 2011/2012 Mhe. Waziri katika muhutasari wake anasema hii paragraph ya kati kati, anasema hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 jumla ya Tanzania shillings milioni tatu nukta sita za SMZ zimetolewa ikiwa ni sawa na asilimia 80.3 ya makadirio, lakini kwa upande wa mashirika ya maendeleo fedha zilizopatikana ni Tanzania Shillings bilioni 21.5 sawa na asilimia, yeye kasema sawa na asilimia 54 lakini kwenye kitabu inasomeke sawa na asilimia 59.

Lakini vile vile katika hapo alipokuwa anaendelea ndipo tulipopotea zaidi Mhe. Spika, yeye anasoma idara, hiyo idara anayosoma humu kitabu tumejaribu kuangalia tumepekua hatuioni.

Sasa Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba hiki kitabu sawa sawa na vitabu vyengine, kitabu hiki kina kurasa 84. Kitabu chake cha mwaka jana tumekiangalia kina kurasa 80 na kakisoma chote. Sasa kitabu cha kurasa 84 kama Mhe. Waziri anasema ni hotuba ndefu hawezi kuisoma yote anasoma kwa muhutasari Mhe. Spika, hii bajeti itakuja kuwa na kipwate hapa.

Sasa ili kumsaidia Mhe. Waziri kwa kuwa hivi vitabu vimeandikwa na vimeandikwa na wizara yake, hili tunaomba bora asome hiki kitabu ili twende sambamba na hizi takwimu anazozisoma vyenginevyo Mhe. Spika, kwa sababu mara nyingi kila mmoja kainamia kitabu.

Sasa ikiwa Waziri maelezo anayoyasoma, maana yake *at least* angetoa kama hivyo unavyosema kwamba kwa taarifa zaidi aangalie ukurasa fulani, sasa hicho hakimo.

Sasa Mhe. Spika, ili tusije tukakusokotana huko mbele na tunataka tumsaidie zaidi Mhe. Waziri kwa sababu hii ndio wizara muhimu, uchumi wa nchi upo kwenye elimu. Sasa ikiwa hapa tunaanza mapema hali kama hii, sijui huko mbele tutakuja kufikia vipi.

Sasa nilikuwa naomba Mhe. Spika, kama itakuwa sio tatizo kurasa 84 sio nyingi, kuna vitabu vinakuja hapa mpaka kurasa 110 na Mawaziri wanasoma. Tunaomba tu kwa kumsaidia Mhe. Waziri. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hili jambo nimelielekeza lipo kwa mujibu wa Kanuni. Ukenda kwenye Kanuni ya 96(2) inatueleza kwamba, "Waziri anayehusika na uwasilishaji wa hotuba ya makadirio ya wizara yake atawasilisha kwenye Baraza hotuba yake kwa ufupi", *underline* kwa ufupi kwa muda usiozidi wa saa mbili.

Sasa inategemea na msomaji kama usomaji wake wa utaratibu inaweza ikachukua muda mkubwa zaidi. Lakini ninachokisema ni kwamba ni kitu ambacho tunakifanya na ni utaratibu wa kawaida, hata ukenda pale Bungeni kitabu ni kikubwa lakini uwasilishaji ninadhani ni dakika 30, kitu kama hicho.

Leo hapa tuna saa mbili ni muda mkubwa sana ili aweze kuelezea vya kutosha. Ninachosema kama kuna tofauti ya asilimia ya kitu kama hicho ulichosema, hiyo itakuwa ni makoseo na Waziri anapaswa kusema kile kilichokuwa sahihi ili Mhe. Mjumbe atakapochangia, wachangie kwa jambo ambalo lipo sahihi kwa mujibu wa hali halisi ilivyo ya utekelezaji.

Lakini kimsingi na zile idara kama hazikupangika sasa nalo itakuwa ni tatizo jengine. Sasa Mhe. Waziri mimi ninataka uhakika hotuba yako hapo ikoje kama inaaendana na kitabu, lakini kama itakuwa inaendana na kitabu na mambo yote yale ambayo unayoyasoma ndivyo yalivyo ndani ya kitabu hapo isingekuwa na tatizo.

Ni zaidi ni ile kutueleza tu na kuelekeza Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu ili kupata maelekezo mazuri unaposoma maelezo Mhe. Waziri na halafu ukatuelekeza kwamba maelezo zaidi yapo kutoka sehemu fulani hadi sehemu fulani, maana yake Waheshimiwa Wajumbe wanaosikiliza kwa makini wakiangalia maeneo hayo na kama ana points ambazo anataka kuchangia baadae bila shaka yale masuala atayakuta yapo kama yalivyo.

Tatizo ni kwamba kama kuna jambo ambalo kuna tofauti ndani ya hotuba hii lakini pia kuna tofauti imetofautiana na kile kilicho ndani ya kitabu, nasema hilo litakuwa ni koseo lilikuwa linahusu liwe limerekebishwa mapema.

Baadhi ya vitabu wakati mwengine kama jambo limeonekana mapema basi karatasi wa kwanza pale huwa kuna karatasi yenye marekebisho kwamba baada ya kupitia mumekuta kumbe kwenye page fulani kuna makoseo na yanaandikwa pale, marekebisho katika page fulani na wakati mwengine Mawaziri huwa pia wanatu-highlight kwamba katika usomaji kutakuwa na marekebisho kwenye sehemu moja, mbili, tatu kwa mujibu alivyopitia baadae na akakuta hayo marekebisho.

Sasa ninachokisema ni kwamba kama hotuba yako unawasilisha imekwenda barabara na kitabu hiki, la muhimu Mhe. Waziri awe anatu-refer maelezo zaidi yapo kutoka ukurasa gani hadi ukurasa gani. Sina hakika kama hilo unaweza ukatuhakikishia hapa hivi sasa kwa mujibu ambavyo mumekaa ndani ya wizara yenu katika kupitia kitabu hiki mukaona kwamba kila kitu kipo sahihi.

Kama hivyo sivyo, sasa hilo siwezi nikatoa jibu mimi kwa sababu ndio tumepewa vitabu punde tu hivi. Kama hivyo sivyo basi ni vyema basi ukasoma hiki kitabu ili yale makoseo na tofauti ziliopo zisije zikazua hoja. Lakini kama una uhakika kitu ulichokiandika hapo ndio sawa na yale yaliomo ndani ya kitabu chetu hiki basi inaruhusika kusoma kwa ufupi, kwa sababu kila tukitumia muda mchache lakini maelezo yakawa wazi yamefahamika itatusaidia kupata wachangiaji wengi zaidi huko baadae kwa sababu mwelekeo umeonesha kwamba mara nyingi wachangiaji hawamaliziki kwa muda ambao tumeweka lakini inabidi wengine tuwakate kuendana na utaratibu ili hatimaye muda uliopangwa kwa mujibu wa Kanuni shughuli yote iwe imemalizika.

Sasa hili sina hakika hiki ambacho Mhe. Hamza amekisema lakini labda na wewe Mhe. Waziri utusaidie baadhi ya hizi takwimu unazozitoa ambazo zimetofautiana ilivyo ndani ya hotuba kama alivyoeleza Mhe. Hamza, basi hilo labda tungelisahihisha au tuka-note down Waheshimiwa Wajumbe ili hatimaye basi hata michango tunaweza tukamuuliza Mhe. Waziri kuna tofauti ya kitu ulichokizungumza ndani ya hotuba lakini kuna tofauti ya kile kilichomo ndani ya kitabu.

Hebu tuhakikishie baadae kipi kipo sawa. Mimi ninadhani hili jambo wala sio tatizo, ni kuhakikisha tu kwamba tunachokisoma ndicho ambacho kimekusudiwa kuwasilishwa mbele ya Baraza hili.

Hivyo Mhe. Waziri hili lipo kwako zaidi, maana wewe ndio mwenye hotuba yako hiyo, hiyo kwa bahati mbaya hakuna aliyekuwa nayo, sisi tuna kitabu hiki, sasa tuone tunakwendaje.

Mhe. Waziri kama huna uhakika wa hotuba hii inakwenda sambamba na hiki basi bora tutumie hiki kitabu, lakini kama una uhakika kwamba kila kitu zile reference unazotu-draw kuziangalia zipo vizuri basi ruksa ninasema ipo na hiyo itakuwa imekwenda kwa mujibu wa Kanuni yetu inavyotuelekeza chini ya Kanuni ya 96 (2).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, sikuwa na nia ya kuingilia lakini naomba nitumie Kanuni hiyo hiyo uliyoitaja ya 96(2), kwa kusaidia tu kwa

sababu ninadhani ni vizuri hasa Mhe. Waziri anaposoma tumpe nafasi ya kusoma kwa utulivu.

Mhe. Spika, mimi ninadhani ikiwa kama ulivyotoa muongozo wako, ikiwa Waziri ana uhakika kwamba hotuba yake ni muhutasari wa kitabu hiki na yaliomo hayapishani kama ulivyosema, na ninadhani kama mwenyewe kajiandaa kusoma huo muhutasari tumpe fursa asome hiyo.

Kwa sababu Mhe. Spika, ninakumbua tumezoea utaratibu huo kwamba hapa na hata uzoefu wangu huko Bungeni, mara nyengine unaweza ukasoma muhutasari lakini mwisho ukasema kwamba katika hansard naomba ichukuliwe ile iliyokuwa imewasilishwa katika kitabu ambayo mara nyingi huwa inaingia yote.

Kwa hivyo ninadhani muhimu ni hizo takwimu kama hazipishani, kama maelezo akafupisha ninadhani tungemruhusu Mhe. Waziri akasoma hotuba yake aliyekuwa anayo, atuthibitishie tu kama mambo mengine yamekwenda sawa sawa kama maelezo ya hayo muhutasari basi tumuache hicho Mhe. Waziri amekiandaa kwa sababu atakuwa amejiandaa vizuri zaidi na pengine atakuwa ana-flow uzuri katika hotuba yake kuliko hivi sasa kumwambia akamate kitabu. Ninaomba Mhe. Spika.

Mhe Spika: Maelezo ya Mhe. Jussa yanalingana na yale ambayo nimeelekeza, kwa hivyo Mhe. Waziri linahusu namna ya hiki ulichokiwasilisha kama hakitofautiani na mambo muhimu yaliomo humu, maana unapotaja takwimu, hicho ni kitu muhimu sana.

Sasa sijui ulijiweka sahihi na watendaji wako kuhakikisha kwamba hotuba hiyo unayosoma haina tofauti kwa sababu kuna baadhi ya tofauti ni very sustentative, ni vitu muhimu ndivyo unavyotaka Waheshimiwa Wajumbe wavielewe ili hatimaye watoe michango yao juu ya haya mambo ambayo umeyasema.

Mhe. Waziri tupe maelezo kidogo ili tupate kuendelea.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa maelezo na maelekezo yako, na ninamshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa ufafanuzi alioutoa ambao unakwenda sambamba na maelekezo yako.

Ninataka nithibitishe binadamu kukosea kupo lakini nina hakika summary iliyofanywa na wasaidizi wangu ime-include contents zote za kitabu changu.

Mimi mwenyewe kitabu changu nimekipata juzi, lakini summary hii ninayo siku nne zilizopita na ndio niliyojiandalia kuwasilisha hotuba yangu.

Ninamuomba sana Mhe. Hamza anivumilie, kama alivyosema ana lengo la kutusaidia na kama alivyosema Wizara ya Elimu ndio wizara muhimu ya maendeleo na uchumi, hili kosa dogo sana lililoonekana hapa lisiwe kikwazo kikubwa. Ninasema ninathibitisha summary tuliyoitengeneza inakwenda sambamba kwa asilimia 99 na yaliomo kwenye kitabu.

Kwa kuwa nimejitayarisha kuwasilisha hotuba yangu kwa kutumia hii summary na mpaka sasa nina-flow vizuri, na ninaomba Mhe. Hamza anivumilie niwasilishe na kama kutatokea hitilafu ndogo ndogo zifute kitabu usizifuate summary, ndivyo nilivyosema na ninaendelea kusema.

Tujadili zaidi kwenye kitabu lakini kitabu nilichokitengeneza kinalingana kwa asilimia 99 na summary.

Mhe. Spika: Uendelee lakini Waheshimiwa Wajumbe kama tunagundua kuna mapungufu *note down* kwenye mchango wako utayasema, waziri baadae atatuwekea wazi kwenye majumuisho.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 35,952,747,000/- kwa Unguja na Tsh. 14,689,253,000/- kwa ofisi iliyoko Pemba.

IDARA YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe. Spika, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, ina majukumu ya kusimamia utoaji wa elimu kwa ngazi ya elimu ya maandalizi na ile ya msingi katika skuli za Serikali na za binafsi. Pia inaratibu shughuli za vyuo vya Kuran na madrasa. Aidha, Idara ina jukumu la kushughulikia huduma za wanafunzi katika skuli.

Elimu ya Maandalizi

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2012, kulikuwa na skuli za maandalizi zilizosajiliwa 253 kati ya hizo 30 ni za Serikali na 223 za binafsi. Pia zipo skuli za msingi 37 ambazo zimeanzisha madarasa ya elimu ya maandalizi. Jumla ya wanafunzi wa skuli za maandalizi wamefikia 31,583 wakiwemo wanawake 16,132 na wanaume 15,451. Kati yao wanafunzi 7,644 wakiwemo wanawake 3,199 na wanaume 3,135 wako katika skuli za Serikali na wanafunzi 23,989 wakiwemo wanawake 12,260 na wanaume 11,679 wako katika skuli za binafsi. Jadweli Namba 13(a) inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika**,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, utoaji wa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio uliendelezwa kupitia programu za Tucheze-Tujifunze. Jumla ya vituo 180 vyenye wanafunzi 3,911 kati yao wanawake ni 1,859 na wanaume 3,096 wanapata elimu ya maandalizi kwa njia ya redio. Vituo hivyo vinasimamiwa na walimu wasaidizi (mentors) 360 ambao wanawaongoza wanafunzi kufuatilia maelekezo yanayotolewa kupitia redio. Kwa kutumia mbinu hii tunaweza kuwapatia elimu ya maandalizi watoto wengi sana walioko vijijini na mijni ambako hadi sasa hakuna skuli za maandalizi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuwapatia watoto elimu ya maandalizi kupitia vipindi vya tucheze- tujifunze ambavyo vinarushwa na kupitia redio ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar. Wizara pia itaendelea na juhudi ya kufungua vituo vyengine katika maeneo mengine ambayo hayana skuli za maandalizi ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu hii. Pia, Wizara inakusudia kufanya marekebisho ya posho za walimu wasaidizi kwa kadri hali itavyoruhusu pamoja na kuvipatia vituo vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, walimu wasaidizi watapatiwa nafasi za kujiendeleza kupitia vituo vya walimu wa maandalizi na mradi wa kuwafundisha walimu kwa njia ya redio.

Mhe. Spika**,** Nachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa mashirika mbali mbali ya Serikali pamoja na watu binafsi kwa kuendelea kuchangia maendeleo ya ngazi hii. Miongoni mwao ni Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC), mashirika ya UNICEF, "*Save the Children*", Jumuiya ya *World Home For Youth"*, "*Zanzibar Madrasa Resource Centre," "Zanzibar Private Madrasa Organisation*", na taasisi zote zinashoghulika na malezi na makuzi ya mtoto.

Elimu ya Madrasa na Vyuo vya Kuran

Mhe. Spika, Idara hii pia, inashughulikia jumla ya madrasa/vyuo vya Kuran 2,251. Aidha zipo jumla ya skuli za maandalizi za madrasa za jamii 84 Unguja na Pemba zinazosimamiwa na kuhudumiwa kupitia Jumuiya ya "*Zanzibar Madrasa Resource Centre*" ambazo ufundishaji wake unafuata misingi ya dini ya Kiislamu. Madrasa/vyuo vya Kuran zimetembelewa na kupatiwa miongozo mbali mbali ya uendeshaji. Katika kipindi hiki, Idara haikuweza kuendesha mafunzo kwa walimu kutokana na ukosefu wa fedha.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu ikishirikiana na Shirika la UNICEF linakusudia kutoa mafunzo kwa walimu wa madrasa/vyuo vya kuran

350. Pia itaendelea kufanya ziara mbali mbali na kutoa ushauri na maelekezo muafaka kwa nia ya upatikanaji wa elimu iliyo bora na sahihi.

Elimu ya Msingi

Mhe. Spika**,** katika mwaka 2011/2012, elimu ya msingi inatolewa katika jumla ya skuli za msingi 155 za Serikali na 39 za binafsi. Aidha idadi ya wanafunzi katika ngazi hii ya elimu ya msingi imefikia 242,229 sawa na asilimia 121.5 ikilinganishwa na wanafunzi 237,690 sawa na asilimia 118.15 ya mwaka 2011. Aidha watoto wote 34,155 walioandikishwa kuanza darasa la kwanza katika skuli za Serikali mwaka huu wa 2012 wamepatiwa nafasi ya kuendelea na masomo yao. Miongoni mwa watoto hao 16,951 ni wanawake na 17,204 ni wanaume. Jadweli Namba. 14 zinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, elimu katika ngazi hii bado inaendelea kukabiliwa na matatizo ya uhaba wa nafasi licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na Wizara kwa ushirikiano na wananchi katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa madarasa, bado tatizo hilo lingalipo. Tatizo hilo ni kubwa zaidi katika Wilaya ya Magaharibi Unguja. Zaidi ya uhaba wa nafasi, elimu katika ngazi hii inakabiliwa na matatizo ya uhaba wa samani na vifaa vya kusomeshea hasa vitabu, na upungufu wa walimu wenye ujuzi na sifa zinazotakiwa kwa baadhi ya Wilaya. Matatizo hayo yamekuwa yakitatuliwa hatua kwa hatua. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imetenga fedha nyingi kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa, uchongaji wa vikalio, ununuzi wa vitabu vya kiada kwa madarasa ya kwanza hadi ya nne na ununuzi wa vifaa vyengine vya kusomeshea. Wizara inawaomba Waheshimiwa Wawakilishi waendelee na juhudi za kuwahamasisha wananchi kuchangia maendeleo ya elimu ya watoto.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali na jumuia zisizo za kiserikali imefanya uchunguzi wa afya za wanafunzi na huduma ya tiba ili waweze kusoma vizuri. Taasisi hizo ni *UNICEF*, "*Save the Children Fund"*, "*Zanzibar Out Reach Programme"* na "*Norwegian Association for Peoples with Development Disabilities*". Pia, shirika la "Save the Children Fund" limekubali kuendelea kufadhili mradi wa uhamasishaji jamii juu ya matumizi ya adhabu mbadala katika skuli baada ya mafanikio ya awamu ya kwanza ambapo kumeonesha kuwa mahusiano na maelewano mazuri kati ya walimu na wanafunzi yamewasaidia wanafunzi kujifunza bila ya hofu ya kupigwa bakora. Katika awamu ya pili, jumla ya skuli kumi (10) zimeongezwa na kufanya idadi ya skuli zote kuwa ishirini (20) ikiwa ni skuli mbili (2) kwa kila Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Idara imeshirikiana na Jeshi la Polisi katika kuanzisha somo la Usalama Wetu kwanza katika skuli 10 za MKoa wa Mjini Magharibi kwa majaribio. Lengo la mpango huo ni kuwawezesha wanafunzi kuzielewa sheria

mbali mbali za nchi, kutambua wajibu wao kwa jamii, kujilinda dhidi ya vitendo vya uvunjaji wa amani na kujilinda dhidi ya vitendo vya unyanyasaji na kuleta ustawi na maendeleo katika jamii.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutatua changamoto zilizopo ili kukuza kiwango cha elimu katika ngazi hii. Pia, Wizara itaendelea kutoa fursa kwa walimu ya kujiendeleza, kuendelea kuzifanya skuli kuwa rafiki na kujenga mahusiano na mashirikiano baina ya skuli za Zanzibar na nje ya Zanzibar. Aidha, Wizara itaweka mkazo katika somo la michezo katika skuli za msingi. Vile vile, mafunzo yatatolewa kwa Serikali za wanafunzi, mafunzo ya mapambano dhidi ya UKIMWI, dawa za kulevya, masuala ya jinsia, mabadiliko ya tabia za nchi na mafunzo ya usalama wetu.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 200,000,000/- kwa Unguja na Tsh. 30,000,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI

Mhe. Spika, Katika mwaka 2011/2012, elimu ya sekondari ilikuwa inatolewa katika skuli 271 kati ya hizo skuli 220 ni za Serikali na 51 ni za watu binafsi. Skuli hizo zilikuwa na jumla ya wanafunzi 81,667 kuanzia kidato cha 1 hadi kidato cha 6, kati yao wanaume ni 38,122 na wanawake ni 43,545. Kwa upande wa sekondari katika ngazi ya elimu ya lazima (kidato cha 1 na kidato cha 2) walikuwepo wanafunzi 51,108 ambao ni sawa na asilimia 86.6 ya watoto wenye umri wa miaka 14-15 wanaotarajiwa kuwepo skuli. Jadweli namba 16 inatoa uchambuzi zaidi. Kwa upande wa ngazi ya elimu ya sekondari ya fursa (kidato cha 3-6) na elimu ya ufundi walikuwepo wanafunzi 30,559. Jadweli namba 20 na 22 zinatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Spika, katika kusambaza huduma ya utoaji wa elimu ya sekondari hasa katika sehemu zote za nchi, na hasa vijijini, Wizara imezifungua skuli mpya za Uzini, Dole na Chaani zilizojengwa kwa mashirikiano na Benki ya Dunia. Skuli hizi zimeanza kwa kuchukua wanafunzi wachache wanaohudhuria masomo kwa mkondo mmoja tu. Skuli hizi zimepatiwa walimu wa kutosha wenye mchanganyiko wa walimu wenye uzoefu na walimu wapya walioajiriwa hivi karibuni, vitabu na vifaa vya maabara na kompyuta. Ni azma ya Wizara kuongeza utoaji wa nafasi za elimu ya sekondari hasa katika skuli za vijijini kwa ajili ya kuwaondoshea usumbufu wa mahali pa kuishi wanafunzi wa skuli za vijijini wanapochaguliwa kuendelea na masomo ya vidato vya tatu na tano katika skuli za mjini.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2012/2013, Wizara inakusudia kuzifungua skuli mpya 10 za sekondari. Pia, inakusudia kuanza tena kuzitumia skuli za sekondari za Forodhani, Tumekuja, Utaani na Fidel Castro ambazo zilifungwa kwa matengenezo makubwa. Kufunguliwa kwa skuli hizo kutasaidia sana kupunguza msongamano wa wanafunzi katika baadhi ya skuli za sekondari.

Serikali za Wanafunzi

Mhe. Spika, Katika mwaka 2011/2012, Serikali za wanafunzi katika skuli zimetekeleza majukumu yake kwa kiwango cha kuridhisha. Serikali za wanafunzi zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwasaidia walimu katika kusimamia kazi za usafi wa skuli, kudumisha nidhamu za wanafunzi na kuwaandaa wanafunzi kwa kazi za uongozi baada ya kumaliza skuli. Wizara imeendesha mafunzo ya viongozi wa serikali za wanafunzi kwa skuli 25 za Unguja na 25 kwa skuli za Pemba. Mafunzo hayo yanahusu historia ya uongozi wa skuli, muundo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na maradhi ya kuambukiza yanayosababishwa na uasharati. Mbali ya serikali za skuli za serikali, vile vile viongozi wa serikali za wanafunzi wa skuli 18 za binafsi walipatiwa mafunzo kama hayo.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 wizara itaandaa mafunzo zaidi kwa viongozi wa Serikali za wanafunzi ili kukuza uweledi wao.

Huduma za Dakhalia

Mhe. Spika, Katika mwaka wa 2012/2013 idadi ya wanafunzi wanaoishi dakhalia ilifikia 1,774 (wanaume 839 na wanawake 917). Idadi hii imeongezeka kidogo ikilinganisha na wanafunzi 1,527 waliokuwepo mwaka 2010/2011. Dakhalia katika skuli ya Fidel Castro na Utaani zimefanyiwa matengenezo, na hivyo kulazimika wanafunzi kuhama na kuishi maeneo mengine kwa muda au na jamaa zao. Ni matarajio ya Wizara kuwa idadi ya wanafunzi watakaohitaji kuishi dakhalia itapungua mara baada ya kufunguliwa kwa skuli za sekondari za kisasa katika sehemu nyingi za vijijini ambazo zitasaidia sana katika kupunguza tatizo la wanafunzi kufuatilia skuli za maeneo ya mijini. Napenda kuwashukuru wazazi na wanadakhalia wote kwa uvumilivu, utulivu na ushirikiano mkubwa wanaouonesha katika kuwahudumia watoto wao. Jadweli namba 24 inatoa uchambuzi zaidi.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2012/2013, Wizara inakusudia kuimarisha huduma za afya katika dakhalia zetu kwa kuweka kisanduku cha huduma ya mwanzo na kuyafanya mazingira ya dakhalia zetu kuwa ya kuvutia zaidi.

Kazi za Ujasiriamali

Mhe. Spika, Katika mwaka 2011/2012, Kazi za ujasiriamali zimeendelea kupewa uzito unaostahiki katika skuli zetu. Pamoja na kuwapa wanafunzi ujuzi na mbinu mbali mbali za uzalishaji mali, skuli zinafaidika kwa kupata fedha ambazo husaidia katika kutatua matatizo madogo madogo yanayozikabili skuli hizo.Skuli zetu nyingi zimewezesha kuendesha miradi ya uuzaji duka, kazi za mikono na kilimo. Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni imeweza kuoainisha mafunzo ya ujasiriamali na masomo ya kawaida. Jitihada zaidi zitaendelezwa kuimarisha mafunzo ya ujasiriamali katika skuli zetu kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 301,000,000/- kwa Unguja na Tsh 38,000,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA ELIMU

Mhe. Spika, Idara hiii ni miongoni mwa Idara mpya zilizoanzishwa mwaka 2011 na inashughulikia masuala yote ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Wizara yangu. Katika mwaka 2011/2012, Idara imeendeleza matayarisho ya sera ya *ICT* katika elimu. Katika kutekeleza zoezi hili, Idara ikishirikiana na *USAID* kupitia mradi wa TZ-21 iliandaa warsha ya siku mbili iliyokuwa na madhumuni ya kupata maoni ya wadau mbali mbali wa elimu wa ndani na nje ya nchi juu ya namna ya kuipitia rasimu ya sera ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika elimu. Michango mbali mbali iliyotolewa itasaidia kurekebisha rasimu ya sera hiyo. Katika mwaka 2012/2013, Idara itakamilisha rasimu ya sera hiyo na kuiwasilisha katika vyombo vya juu vya Serikali.

Mhe. Spika, Idara kwa kushirikiana na *USAID* inatekeleza mradi mkubwa wa kutumia kompyuta kama ni chombo cha kujifunza na kusomeshea ("TZ-21"). Kwa kupitia mradi huu, jumla ya skuli 248 za msingi na vituo 10 vya ualimu vitafaidika na huduma za mradi huu. Kati ya hizo skuli 25 zitaingia katika "*bridge IT*" na skuli 20 zitaingia katika "*Mobile Lab*". Utekelezaji wa mradi huu umeanza kwa majaribio katika skuli mbili za Kisiwandui na Darajani pamoja na Kituo cha Walimu cha Michakaeni. Skuli hizi na Kituo zimepatiwa kompyuta na vifaa vyengine muhimu kwa ajili ya kufanyiwa majaribio.

Mhe. Spika, Mradi huu unategemewa kutoa nafasi kwa walimu kutumia njia shirikishi za kusomeshea na za kisasa katika madarasa yao. Lengo kuu la mradi ni kuimarisha utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT*)

katika usomeshaji wa wanafunzi wa skuli za msingi za hapa Zanzibar. Miongoni mwa vipengele vya mradi ni utoaji wa mafunzo kwa walimu juu ya njia shirikishi za kusomeshea katika masomo ya Hisabati, Sayansi na Lugha kwa madarasa ya I-IV. Kutolewa mafunzo kwa walimu juu ya utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ufundishaji na uendeshaji wa skuli na kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ili kuimarisha mazingira muafaka katika skuli, wilaya na Wizara kwa ujumla.

Mhe. Spika, Idara iliandaa mafunzo ya walimu wasaidizi wanaosimamia vituo vya utoaji wa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio na darasa la kwanza hadi la pili. Jumla ya washiriki 89 wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa vituo vya Tucheze-Tujifunze, kati ya hao 48 ni kutoka Pemba na 41 kutoka Unguja. Pamoja na hayo washiriki walipata kujuana na wenzao kutoka vituo mbali mbali vya Unguja na Pemba jambo ambalo limeweza kujenga mshikamano ulio mzuri katika kuleta ubora wa utendaji kazi hasa katika sekta ya elimu.

Mhe. Spika, Idara imeendelea kuweka taarifa mbali mbali katika tovuti ya Wizara yenye anuani www.moe-z.go-tz. Taarifa zilizoko katika tovuti hiyo ni pamoja na matokeo ya mtihani wa kidato cha pili na machapisho mbali mbali ya sera na mipango ya Wizara. Katika mwaka 2012/2013, Idara itaongeza taarifa zitakazowekwa katika tovuti na pia itaanzisha anuani za barua pepe kwa kila Idara na vitengo ili zitumike kwa mawasiliano ya kiofisi na kuepusha kutumia anuani za barua pepe za mtu binafsi kwa shughuli za kikazi.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2012/2013 Idara inakusudia kuikamilisha rasimu ya Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano pamoja na kutayarisha mpango mkakati wa miaka mitano, kuandaa mafunzo kwa watendaji wa Wizara, kuimarisha njia za mawasiliano na usambazaji wa taarifa kupitia Teknohama, kuimarisha tovuti ya Wizara, kutayarisha “database” ya watumishi wa Wizara na kuimarisha matumizi ya Teknohama kwa walimu na watendaji wa Wizara.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara hii imepangiwa kutumia Tsh 120, 00,000/- kwa Unguja na Tsh 21,000,000/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA ELIMU MBADALA NA WATU WAZIMA

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kuondoa tatizo la kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wananchi wa visiwa hivi. Pia ina jukumu la kuwapatia elimu mbadala vijana walioacha masomo njiani na wale ambao hawakuwahi kwenda skuli kabisa kwa kutoandikishwa.

Kisomo

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, juhudi za kuhamasisha wananchi ambao hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu, kufungua na kujiunga na madarasa ya kisomo zimechukuliwa na kufanikiwa. Jumla ya madarasa 10 mapya ya kisomo yamefunguliwa katika sehemu mbali mbali za mjini na vijijini Unguja na Pemba. Idadi ya madarasa ya kisomo yameongezeka kutoka 47 mwaka 2010/2011 na kufikia madarasa 57 mwaka 2011/2012 yenye jumla ya wanakisomo 6,492, wakiwemo wanawake 5,689 na wanaume 803. Jumla ya wanakisomo 6,029 (wanawake 5,240) wamefanyiwa upimaji katika hatua zote nne. Katika upimaji huo jumla ya wanakisomo 444 wakiwemo wanawake 362 wamekombolewa. Jadweli Namba. 35 inatoa ufafunuzi zaidi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara itaendelea na juhudi zake za kushajiisha na kuhamasisha wananchi ambao hawajui kusoma na kuandika, kufungua na kujiunga katika madarasa ya kisomo hasa katika maeneo ambayo yana idadi kubwa ya wananchi wasiojua kusoma na kuandika.

Elimu Mbadala

Mhe. Spika, Elimu Mbadala inalenga kuwapatia elimu vijana wenye umri kati ya miaka 10 hadi 15 walioko nje ya skuli, wakiwemo walioacha masomo njiani kutokana na sababu mbali mbali. Katika mwaka 2011/2012, Elimu Mbadala imetolewa katika madarasa 28 Unguja na Pemba yakiwa na jumla ya wanafunzi 711 (Pemba wanafunzi 265 na Unguja wanafunzi 446). Kati ya wanafunzi hawa wanawake ni 224 na wanaume 487.

Mhe. Spika, Kituo cha Elimu Mbadala cha Rahaleo Zanzibar kina jumla ya wanafunzi 243 wanawake 62 na wanaume 181. Wanafunzi wa kituo hiki ni vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 20. Kituo hiki pamoja na kusomesha masomo ya kawaida pia wanafunzi wanajifunza fani mbali mbali zikiwemo ushoni, upishi, utalii, umeme na uchongaji.

Mhe. Spika, jumla ya wanafunzi 49 wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Rahaleo, wakiwemo wanaume 35 na wanawake 14 wa fani za umeme, uchongaji na utunzaji wa nyumba wamemaliza mafunzo yao na kutunukiwa vyeti. Vijana hao wengi wao tayari wamepata ajira katika taasisi mbali mbali hapa nchini na wengine wamejiajiri wenyewe.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Idara inakusudia kuongeza idadi ya vijana wa kujiunga na madarasa ya elimu mbadala katika skuli za msingi na pia kuongeza wanafunzi katika Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo.

Vituo vya Kujiendeleza

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012 jumla ya wanafunzi 3,576, kati yao wanawake 1,827 na wanaume 1,749 wamesajiliwa katika vituo mbali mbali vya kujiendeleza Unguja na Pemba. Jadweli Namba. 36 linatoa ufafanuzi zaidi.

Aidha katika mwaka huo huo, wanafunzi 11,854 wamefanya mtihani wa faragha (kidato cha IV) na wanafunzi 7,694 wamefaulu, sawa na asilimia 64.9 ya watahiniwa wote. Kwa upande wa kidato cha sita, jumla ya vijana 993 wametahiniwa, wasichana 568 na wavulana 425. Kati yao 301 wamefaulu sawa na asilimia 30.3. Jadweli Namba 37 (a-c) na 38 (a-c) zinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Idara itafungua vituo zaidi vya kujiendeleza kila itakapohitajika.

Programu za Wanawake

Mhe. Spika, Idara hii pia ina jukumu la kuwahamasisha wananchi na hasa wanakisomo ambao wamemaliza hatua ya nne kufungua na kujiunga na vikundi vya programu za wanawake. Idara inasimamia vikundi 53 vya programu za wanawake, ambavyo 33 kati ya hivyo viko Unguja na 20 Pemba. Vikundi hivyo vina jumla ya kinamama 1,517.

Mhe. Spika, katika suala zima la kuviendeleza na kuviimarisha vikundi hivyo, Idara imevitunuku vyarahani vikundi 10 ambavyo vimejitokeza kuwa vikundi bora katika kila Wilaya za Unguja na Pemba. Aidha viongozi wa vikundi hivyo wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali kwa lengo la kuendeleza shughuli zao za kazi.

Vyombo vya Habari

Mhe. Spika, Idara inatumia vyombo vya habari katika kuendeleza kisomo cha watu wazima. Kwa mwaka 2011/2012, Idara imefanikiwa kurusha hewani vipindi 13 vya redio kwa Unguja na vipindi 7 kwa Pemba. Pia ilirusha hewani vipindi 6 vya televisheni kwa Unguja na vipindi 3 kwa Pemba. Aidha, Idara iliandaa makala 4 zilizochapishwa katika gazeti la Zanzibar Leo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Idara itaendelea na juhudi za kuwaelimisha wanakisomo kwa kutumia vyombo vya habari nchini pamoja na kuzitumia maktaba zilizopo mjini na vijijini ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 202,000,000/- kwa Unguja na Tsh 25,000,00/- kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MAFUNZO YA UALIMU

Mhe. Spika, Idara ina jukumu la kusimamia mafunzo ya ualimu vyuoni na mafunzo ya ualimu kazini kupitia vituo vya walimu.

Mhe. Spika, Vyuo vyetu vya ualimu vitatu; ambavyo ni Chuo cha Kiislamu Unguja (Mazizini), Chuo cha Kiislamu Pemba (Micheweni) na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa Pemba viliendelea kuendesha mafunzo ya ualimu. Kwa mwaka 2011/2012, vyuo hivyo vilikuwa na jumla ya wanafunzi 516 kati yao wanaume ni 161 na wanawake 355. Kati ya wanachuo hao, 72 ni wanasomea Stashahada ya Ualimu Sekondari, 188 ni wa Stashahada ya Ualimu Msingi na 256 Stashahada ya Dini na Kiarabu. Jadweli Namba 30 (a-c) zinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, Vyuo vya Ualimu vitaendelea kutoa mafunzo ya ualimu kwa kuandikisha wanafunzi wapya katika ngazi ya stashahada ya ualimu msingi, stashahada ya ualimu sanaa sekondari, stashahada ya Dini na Kiarabu na cheti cha elimu mjumuisho. Taratibu za kuviwezesha vyuo kuchukua wanafunzi wapya katika mwaka mpya wa masomo zimeandaliwa na zinatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Mhe. Spika, Idara imepitia na kuandaa mtaala mpya wa mafunzo ya stashahada ya ualimu wa elimu ya msingi. Mihutasari ya masomo 19 imetayarishwa na itaanza kutumika rasmi kwa mwaka wa masomo wa 2012/2013. Katika mtaala huo ufundishaji utaelekezwa zaidi katika kutoa mbinu za kufundisha ueledi "*competency based education".* Pia, masomo mapya ya *TEHAMA* (*ICT*), elimu mjumuisho, michezo na sanaa yameingizwa katika mtaala huo. Mbali ya kusomesha somo la *TEHAMA* kama ni somo kamili, pia wanachuo watasomeshwa matumizi ya *TEHAMA* kama ni nyenzo ya kusomeshea kwa kila somo.

Mhe. Spika, Wizara imeviimarisha Vyuo vya Ualimu ili viweze kutoa elimu bora. Wizara imevipatia vyuo walimu wenye ujuzi, vifaa na usafiri. Awamu ya pili ya ujenzi wa kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchanga Mdogo inaendelea vizuri na kazi zinatarajiwa kukamilika na chuo kutumika katika mwaka wa masomo wa 2012/2013.

Vile vile hatua zimechukuliwa za kukiimarisha Chuo cha Kiislamu, Mazizini kwa kuanzisha ujenzi wa jengo lenye ukumbi wa kisasa na uchimbaji wa

kisima cha maji. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Benki ya Watu wa Zanzibar kwa msaada wao wa Tsh. 50,000,000/= kwa hatua ya awali katika ujenzi wa ukumbi wa kisasa. Pia natoa shukrani zangu kwa shirika lisilo la kiserikali la "*REHEMA FOUNDATION*" kwa msaada wa uchimbaji wa kisima cha maji.

Mafunzo ya Ualimu Kazini

Mhe. Spika, Idara imeandaa rasimu ya Sera ya Mafunzo ya Ualimu kazini. Sera hii itatoa muongozo wa namna ya uendeshaji wa mafunzo kazini, washiriki wa mafunzo na muda wa mafunzo hayo. Pia sera itaweka muongozo wa namna mwalimu atavyonufaika kimaslahi kwa kuhudhuria muda kadhaa wa mafunzo ya ualimu.

Mhe. Spika, Idara pia, imeendelea na utoaji wa mafunzo ya ualimu kwa njia ya elimu masafa kwa walimu wa skuli za msingi wasiosomea ualimu. Walimu 675 wakiwemo wanaume 119 na wanawake 556 walimaliza mafunzo katika ngazi ya daraja la III B, mwezi Julai 2011 kwenye vituo vyote tisa vya walimu vya Unguja na Pemba. Walimu hawa sasa wanaendelea na mafunzo ya daraja la III A. Katika mwaka 2012/2013, Idara itaendelea na utoaji wa mafunzo ya ualimu kwa njia ya elimu masafa kwa walimu 500 wasiosomea. Halikadhalika vituo vya walimu wa maandalizi viwili vitaendelea kutoa mafunzo ya awali kwa vijana wenye hamu ya kusomea ualimu wa maandalizi.

Mhe. Spika, Wizara inakusudia kuinua uwezo wa walimu kufundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Idara, imeandaa mafunzo kazini kwa walimu wataofundisha masomo ya madarasa ya tano na sita kwa lugha ya Kiingereza kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Jumla ya walimu 468 kati yao walimu wanawake walikuwa ni 276 na wanaume walikuwa 192 wanaosomesha madarasa ya tano na sita walihudhuria mafunzo ya kuinua uwezo wao wa kusomesha kwa kutumia Lugha ya Kiingereza.

Mhe. Spika, pia walimu 500 wanaofundisha Sayansi na Hisabati wa madarasa la tano na sita walipatiwa mafunzo ya kufundisha kwa kutumia lugha ya Kiingereza.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, idara itaendesha mafunzo kwa walimu 150 wanaofundisha masomo ya Hisabati na Sayansi kwa darasa la tano na sita. Pia, idara kwa kushirikiana na Shirika la *UNICEF* itaandaa mafunzo kwa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa madarasa ya 1 hadi 4. Uandishi wa moduli za walimu wa Sayansi umeanza na hatua za kumtafuta Mshauri Mwelekezi, ambaye ataongoza uandishi wa moduli na kuendesha

mafunzo ya Hisabati zinaendelea. Maelezo zaidi Kuhusu Idara ya Mafunzo ya Ualimu yanatolewa katika ibara ya 106 hadi 110.

Mhe. Spika, kwa kuimarisha ufundishaji kwa kutumia lugha ya Kiingereza katika ngazi ya sekondari, Idara kwa kushirikiana na "*British Council*" imetoa mafunzo ya matumizi ya Kiingereza kwa wakufunzi 22 kutoka katika Vyuo vya Ualimu na Vituo vya Walimu. Jumla ya walimu wanaofundisha skuli za sekondari 220 wamepatiwa mafunzo hayo. Pia idara iliendesha mafunzo ya mbinu za ufundishaji wa lugha ya Kiingereza cha mawasiliano kwa walimu 90 kati yao 50 katika kituo cha Walimu Dunga na walimu 40 katika kituo cha Walimu cha Wingwi.

Mafunzo hayo yalidhaminiwa na Ubalozi wa Marekani nchini ambao ulitoa msaada wa vifaa mbali mbali. Katika mwaka 2012/2013, Idara itaendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya Kiingereza kama ni lugha ya kufundishia kwa walimu wa sekondari. Mafunzo yataendeshwa na wakufunzi waliopata mafunzo chini ya mradi ulioendeshwa na "*British Council*".

Mhe. Spika, wizara imeweka mkazo mkubwa katika ufundishaji wa masomo Sayansi na Hisabati. Walimu 30 kutoka skuli 15 za Unguja wanaofundisha somo la Physics walipata mafunzo ya jinsi ya kutumia '*Micro laboratory kits'*. Vifaa hivyo vilitolewa msaada na Shirika la *UNESCO*. Mafunzo kama hayo yatatolewa pia kwa walimu wa somo la *Physics* kwa skuli za Pemba katika mwaka huu. Hadi sasa skuli 25 tayari zimefaidika na mpango huu.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara itawaendeleza walimu wanaosomesha masomo ya sayansi madarasa ya sekondari ambao wamemaliza kidato cha sita, *FTC* na Ualimu daraja la IIIA kwa awamu wa pili ya mradi wa "*Teacher Advancement Program"* (*TAP*). Walimu hawa wamesaidia sana kupunguza uhaba wa walimu wa Sayansi na Hisabati katika skuli zetu.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, wizara inakusudia kuviimarisha Vituo vya Walimu kwa kukamilisha ujenzi wa baadhi ya majengo yake ambayo yatasaidia kuvipatia vituo nafasi ya kutosha ya kuendesha mafunzo mbali mbali. Kutokana na uhaba wa nafasi uliopo hivi sasa, baadhi ya mafunzo yanaendeshwa katika madarasa ya skuli jirani jambo ambalo huleta usumbufu.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, idara kupitia mradi wa Tz -21, itaendesha mafunzo kwa walimu wanaosomesha madarasa ya 1 hadi 4. Mafunzo hayo yatahusu namna ya kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufundisha, namna ya kutumia "*e-book*" na kufundisha walimu mbinu za usomaji wa vitabu vya hadithi ili kukuza uwezo wa usomaji kwa wanafunzi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, idara hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 220,000,000/= kwa Unguja na shilingi 28, 000,000/= kwa Pemba kwa kazi za kawaida.

OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU:

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ina jukumu la kuzikagua Skuli zote za Serikali na za Binafsi. Pia, ina jukumu la kutoa mafunzo mafupi na maelekezo kwa walimu wakuu juu ya namna ya kuziongoza skuli zao.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya skuli 287 zilikaguliwa na kupindukia lengo la kukagua skuli 190. Pia, Walimu Wakuu 140 kutoka Skuli za Serikali na za Binafsi, Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo ya uongozi kwa muda wa wiki moja.

Aidha, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu ilifanya ufuatiliaji wa mafunzo yaliyotolewa kwa walimu wakuu katika skuli 62 na matokeo yake yameonesha kuwa kuna mabadiliko katika utendaji wa skuli hizo. Pia, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu, kwa ushirikiano na Shirika la *UNICEF* ilichapisha vijitabu 200 vya viwango vya elimu ya msingi (*education standards*). Katika kuwaendeleza Wakaguzi, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu iliandaa mafunzo ya awali kwa wakaguzi wanane wapya na wakaguzi wawili walihudhuria mafunzo ya matumizi ya kompyuta. Maelezo zaidi katika ukaguzi huo wa elimu yanatolewa kwenye ibara ya 113 hadi 114.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ina lengo la kukamilisha rasimu ya sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu. Pia ina lengo la kuzikagua skuli 300. Kati ya hizo skuli 30 zitafanyiwa ukaguzi mkuu, skuli 100 ukaguzi wa ziara, skuli 36 ukaguzi wa ufuatiliaji, skuli 17 ukaguzi wa usajili, skuli 100 ukaguzi wa ziara ndogo ndogo na skuli 17 ukaguzi maalum. Ofisi pia inakusudia kufanya Ukaguzi Mkuu wa wastani wa skuli mbili za Msingi na Sekondari kwa wakati mmoja.

Vile vile ofisi inakusudia kufanya ukaguzi wa ziara kwa skuli mbili kwa siku moja au kwa wakati mmoja. Pia Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu inategemea kuwasilisha viwango vya elimu kwa walimu wakuu kwenye vituo vyao vya walimu na kuwakabidhi kopi za vijitabu vya viwango hivyo pamoja na vipeperushi na vibango. Kopi za tafsiri ya Kiswahili pia zitachapishwa na kugawiwa.

Kazi ya kusimamia uongozi wa skuli pia itaendelezwa kama ajenda muhimu ya shughuli za ofisi. Ofisi pia imepanga kuendelea kuandaa na kutoa mafunzo kwa Wasaidizi Walimu Wakuu kwa skuli za Serikali na baadhi ya skuli za

binafsi. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu vile vile imepanga kufanya ziara Tanzania Bara kwa baadhi ya wakaguzi, ambako watajifunza mbinu za madaraka mikoani katika tasnia ya ukaguzi wa skuli. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu, pia itarekebisha mpangilio wa ukaguzi wa skuli.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu imepangiwa ruzuku ya shilingi 90,000,000/= kwa kazi za kawaida.

TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR:

Mhe. Spika, Taasisi ya Elimu Zanzibar ina majukumu ya kutayarisha mitaala na mihutasari ya masomo, utungaji na uchapishaji wa vitabu na usanifu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, taasisi ilirekebisha mihutasari mipya ya Elimu ya Maandalizi na kwa sasa mihutasari hiyo inafanyiwa uhariri kabla ya kuchapishwa na kutumika rasmi katika skuli zote za maandalizi. Vile vile taasisi ilishirikiana na Idara ya Mafunzo ya Ualimu kupitia na kurekebisha mtaala wa stashahada ya ualimu msingi pamoja na kutayarisha mihutasari ya masomo yake.

Mhe. Spika, taasisi iliendelea kutoa mafunzo ya awali ya matumizi ya mihutasari mipya ya msingi kwa walimu wa darasa la tatu. Pia Taasisi ya Elimu Zanzibar ilisambaza vifaa vya maabara kwa skuli za sekondari 4, vyuo vya Ualimu 2 na Vituo vya Walimu 10. Aidha, vifaa vya maabara viligaiwa kwa skuli za sekondari 17 Unguja na Pemba zilizofanya mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne. Pia Taasisi ilitayarisha vigezo vitakavyotumika katika uchapishaji wa vitabu vya miongozo ya wanafunzi na vya walimu kwa madarasa ya kwanza hadi ya nne.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Taasisi ya Elimu itachapisha na kusambaza vitabu vya wanafunzi na miongozo ya walimu kwa madarasa ya kwanza hadi darasa la nne. Pia itaandika, kuchapisha na kusambaza vitabu vya wanafunzi na miongozo ya walimu kwa skuli za maandalizi.

Pia, taasisi itaendelea na kuandaa Mpango Mkakati wa Taasisi ya Elimu Zanzibar, itaandaa mtaala wa cheti cha ualimu kwa mafunzo ya uwalimu wa maandalizi, itapitia na kufanya marekebisho ya mihutasari ya Dini na Kiarabu ya Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada katika Vyuo vya Kiislamu.

Vile vile inakusudia kutoa mafunzo ya awali juu ya matumizi ya mihutasari mipya ya *Diploma* ya Msingi kwa wakufunzi na Vyuo vya Ualimu na kuendelea kutoa mafunzo kwa walimu wanaosomesha darasa la nne juu ya

matumizi ya muhtasari mpya wa elimu ya msingi. Katika kuwaendeleza wanafunzi wa sekondari kupenda masomo ya sayansi, taasisi inakusudia kuendesha Kambi ya Mafunzo ya Sayansi na kuandaa Mashindano ya Masomo ya Sayansi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, taasisi hii imepangiwa ruzuku ya shilingi 72,000,000/= kwa kazi za kawaida.

MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI:

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ina majukumu ya kutoa, kusimamia na kuratibu shughuli zote za elimu na mafunzo ya amali hapa Zanzibar. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya wanafunzi 730 kati yao 175 ni wanawake na 555 ni wanaume wanapatiwa mafunzo ya kazi za amali katika Vituo vitatu vya Mafunzo ya Amali vya Serikali.

Vijana hawa wanajifunza katika fani mbali mbali za ufundi zikiwemo useremala, ushoni, uhunzi, upishi, uchoraji na uandishi wa alama, uashi, ufundi bomba, teknolojia ya habari na mawasiliano, huduma za chakula na vinywaji, elektroniki, ufundi magari, umeme na ufundi mafriji na viyoyozi. Jadweli Namba 40 (a) inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, Mamlaka pia inaratibu shughuli mbali mbali za maendeleo ya mafunzo ya amali ikiwemo Mitihani ya Taifa ya Uhasibu na Biashara (*NABE*), Mitihani ya ufundi stadi "*Trade Test*" na "*Competency Based Education and Training*" (*CBET*) inayotahiniwa na Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi (*VETA*) ya Tanzania Bara. Jumla ya vijana 1,391 walifanya mitihani hiyo kati yao 965 walifaulu ikiwa ni sawa na asilimia 69.4. Maelezo zaidi kuhusu mafunzo ya amali yanatolewa na ibara ya 122 hadi 123.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2012/2013 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imepanga kuimarisha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na kuimarisha utoaji wa mafunzo ya amali. Katika kufikia malengo makuu hayo Mamlaka imepanga kutekeleza mambo yafuatayo :-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya mwaka 2005 na Sheria ya Mafunzo ya Amali namba 8 ya 2006 kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 11 ya 2007.

(ii) Kuanza ujenzi wa Ofisi kuu ya Mamlaka kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali II.

(iii) Kuijengea uwezo wa kiutendaji Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Bodi yake ya Wakurugenzi.

(iv) Kuzifanyia marekebisho Sera ya Elimu ya Amali na Mafunzo ya mwaka 2005 na sheria ya Mafunzo ya Amali namba 8 ya mwaka 2006.

(v) Kuimarisha zaidi Mamlaka kwa kuongeza wafanyakazi, kuipatia vifaa na zana za kutendea kazi na usafiri wa uhakika ili kuiwezesha kufanya kazi za ufuatiliaji, kutoa mafunzo na shughuli zake nyengine kwa ufanisi zaidi.

(vi) Kuongeza utaalamu, ujuzi na uwezo wa wafanyakazi na walimu wa Mamlaka kwa kuwapatia mafunzo kwa mujibu wa kazi na fani zao ndani na nje ya nchi.

(vii) Kuimarisha divisheni mpya ya Mitihani na Tathmini kwa kuipatia wafanyakazi na vifaa vya kutendea kazi.

(viii) Kuendelea kusajili vituo vinavyotoa mafunzo ya amali vya Zanzibar vya umma na vya binafsi.

(ix) Kutoa, kusimamia na kuratibu mafunzo ya amali kwa vijana 3,400 katika vituo mbali mbali vya mafunzo ya amali ndani na nje ya nchi.

(x) Kuandaa mtihani wa pamoja kwa vituo vyote vinavyotoa mafunzo ya amali hapa Zanzibar kwa kuanzia na vituo vinavyomilikiwa na Mamlaka.

(xi) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za maisha kwa wakufunzi na wafanyakazi wa Mamlaka na Wanafunzi kwa Vituo vya Mafunzo ya Amali.

(xii) Kutoa huduma za mafunzo na vifaa kwa vituo vya mafunzo ya amali vilivyosajiliwa rasmi na Mamlaka.

(xiii) Kuimarisha uzalishaji na uwekezaji ili kuongeza mapato ya Mamlaka.

(xiv) Kuendeleza uhusiano na mashirikiano kati ya Mamlaka na mashirika ya Kitaifa, kikanda na Kimataifa yanayohusiana na Mafunzo ya Amali kwa kuhudhuria mikutano, makongamano na warsha mbali mbali zinazojadili maendeleo ya mafunzo ya amali.

Mhe. Spika. kwa mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imepangiwa ruzuku ya shilingi 2,200,000,000/= kwa kazi za kawaida.

TAASISI ZA ELIMU YA JUU

Mhe. Spika, hadi sasa tunazo Taasisi nne za Elimu ya Juu hapa Zanzibar ambazo shughuli zake zinaratibiwa na wizara yangu. Kati ya taasisi hizo, mbili zinamilikiwa na SMZ ambazo ni Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Mbili zilizosalia zinamilikiwa na taasisi binafsi ambazo ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani na Chuo Kikuu cha Zanzibar.

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR:

Mhe. Spika, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimetimiza miaka kumi tokea kuanzishwa kwake. Katika kipindi hicho, kimepata mafanikio makubwa. Chuo kilianza na wanafunzi 52 tu wa shahada ya kwanza katika Fani ya Sanaa na Ualimu. Hivi sasa chuo kinatoa mafunzo ya Shahada na Stashahada ya Sayansi na Ualimu pamoja na Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mawasiliano.

Kwa mwaka 2011/2012 chuo kina jumla ya wanafunzi 1,440 ambao 702 ni wanawake sawa na asilimia 49 ya wanafunzi wote. Wanafunzi wa ngazi ya shahada wapo 782, wa ngazi ya stashahada ni 614 na wa ngazi ya cheti ni wanafunzi 44. Jadweli Namba 26(a) inatoa ufafanuzi. *(Makofi)*

Pia Chuo kupitia taasisi yake ya elimu endelevu hutoa huduma za kuwapatia elimu wananchi katika fani mbali mbali zikiwemo za mambo ya Utalii, Ukutubi, Kompyuta na lugha ya Kiingereza.

Mhe. Spika, Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar mbali na kutoa mafunzo ya stashahada ya lugha, pia hufundisha Kiswahili kwa wanafunzi wa kigeni. Kwa mwaka wa 2011/2012, jumla ya wageni 126 (wanaume 30 na wanawake 96) wamejiunga na TAKILUKI kujifunza lugha za Kiswahili.

Mhe. Spika, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kilifanya mahafali yake ya saba tarehe 24 Disemba, 2011. Mkuu wa Chuo hicho ambae ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein aliwatunuku shahada, stashahada na vyeti wahitimu katika fani mbali mbali.

Katika mahafali hayo jumla ya wahitimu 327 wakiwemo wanawake 155 walitunukiwa shahada, stashahada na vyeti. Kati yao, wanafunzi 139 walikuwa wa shahada ya kwanza ya sanaa na elimu, wahitimu 63 walikuwa ni wa fani ya sayansi na elimu na wahitimu 11 wa shahada ya sayansi ya kompyuta. Kwa ngazi ya stashahada, wahitimu 82 walitunukiwa stashahada ya lugha na elimu na 18 wa fani ya Sayansi ya Kompyuta. Pia wahitimu 14 walitunukiwa vyeti katika fani ya Sayansi ya Kompyuta. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa *SUZA* imeanzisha madarasa ya sekondari ya mchepuo wa sayansi katika kampasi ya Nkrumah. Skuli hii imeanzia na wanafunzi 45 wa kidato cha tano ambao kati yao 13 ni wanawake. Lengo la kuanzisha madarasa hili maalum, ni kuwaandaa mapema vijana wenye mwelekeo wa masomo ya sayansi, ambao baadae watachangia katika kupunguza tatizo la uhaba wa wahitimu wa masomo ya sayansi, ambao unapelekea kuwa na uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi kwenye skuli zetu. Maelezo zaidi Kuhusu Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar yanatolewa katika ibara ya 126 hadi 131.

Mhe. Spika, Chuo katika mwaka wa 2011/2012 kimeweza kuimarisha mashirikiano yake na taasisi na vyuo vikuu mbali mbali vya kigeni. Miongoni kwa vyuo hivyo Chuo Kikuu cha Taifa cha South Carolina cha Umarekani, Edward Mondlane cha Msumbuji, Chuo Kikuu cha Humboldt cha Ujerumani na Chuo Kikuu cha Bristol cha Uingereza.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Chuo Kikuu cha Taifa kitaendelea kuimarisha shughuli zake zaidi kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuendelea kuchukua wanafunzi wapya katika fani na viwango mbali mbali. Chuo kinakusudia kufanya mageuzi makubwa na kuanzisha skuli mpya kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu hicho. Chuo pia kinatarajiwa kuhamishia shughuli zake katika kampansi ya Tunguu.

Mhe. Spika, naomba kutoa shukrani za dhati na pongezi nyingi kwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Dkt Ali Mohammed Shein kwa kuwa karibu na Chuo na kwa Uongozi na ushauri wake wa busara ambao umekisaidia Chuo kufikia hapo tulipo. Napenda pia kutoa pongezi na shukrani

kwa Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Hassan Nassor Moyo kwa uongozi mzuri ambapo imekiwezesha chuo kupata mafanikio makubwa katika kipindi kifupi.

Vile vile nawapongeza na kuwashukuru viongozi wakuu wote wa Chuo Kikuu cha Taifa pamoja na watendaji wake wote wakiwemo wahadhiri, wakufunzi, wafanyakazi wengineo na wanafunzi wote kwa mashirikiano yao mazuri ambayo yamewezesha jumuiya ya chuo kuishi kwa amani, udugu na utulivu mkubwa. Ni matumaini yangu kwamba nidhamu hii iliyooneshwa na Chuo Kikuu cha Taifa itaendelea kudumu na hivyo kukiwezesha chuo kutimiza malengo yanayotarajiwa na Taifa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, chuo hiki kimetengewa ruzuku ya shilingi 4,200,000,000/= kwa kazi za kawaida.

TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mhe. Spika, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ni Taasisi inayojitegemea na inajukumu la kufundisha fani za ufundi, sayansi na teknolojia katika ngazi ya stashahada. Taasisi ina malengo la kutoa mafunzo ya stashahada ya juu na shahada ya kwanza katika fani za ufundi na teknolojia hapo baadae.

Mhe. Spika, taasisi inajukumu la kupanga malengo ya muda mfupi na muda mrefu yatakayoiwezesha Taasisi kujiendesha wenyewe mbali ya kupata ruzuku kutoka serikalini.

Baraza la Taasisi limekutana vikao kumi na moja na maagizo thelathini na moja yalitolewa na kutekelezwa. Baraza liliweza kusimamia vizuri utekelezaji wa malengo kumi na nne yaliyowekwa mwaka 2011/2012, ambapo kati ya malengo hayo, malengo kumi na mbili yalitekelezwa kwa ufanisi mkubwa na baadhi yao kuvuka lengo lililowekwa.

Kwa mfano, taasisi ilitengeneza vikalio 160 badala ya 80 na kuondoa kabisa tatizo la vikalio pale skuli na sio nchini. Katika mwaka wa masomo 2011/2012 Taasisi ilisajili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 172 badala ya 100 na kufanya idadi ya wanafunzi wote kwa mwaka huu wa masomo kufikia 336 na kuvuka lengo la wanafunzi 300 ifikapo 2012. Jadweli Namba 29 inatoa ufafanuzi zaidi.

Idadi ya wakufunzi waliopo masomoni iliongezeka kutoka watatu hadi sita na tayari wakufunzi 4 wameshaomba kufanya shahada ya uzamivu katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha mwaka wa masomo 2012/2013.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, taasisi inakusudia kuendeleza malengo yaliyowekwa katika mpango kazi na kuweka msisitizo na inakusudia kufanya uhakiki wa mali za taasisi (*fixed asset value*), kuanzisha mafunzo ya stashahada ya Mawasiliano ya Habari na Biashara (*Diploma in ICT with Business*), kutayarisha mihutasari ya mafunzo ya walimu wa Sayansi na Hisabati kwa skuli za sekondari katika ngazi za cheti na stashahada pamoja na kuanza kutoa mafunzo hayo.

CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR:

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2011/2012, Chuo Kikuu cha Zanzibar kina jumla ya wanafunzi 2,162 kati yao wanaume 1122 na wanawake 1040. Wanafunzi 424 wanasomea shahada ya kwanza ya sheria na shari'a, 253 shahada ya biashara na masoko, 400 shahada ya uongozi wa umma, 132 shahada ya uchumi na 97 wa shahada ya sayansi ya kompyuta. Pia, wapo wanafunzi 696 wa masomo ya ngazi ya stashahada na wanafunzi 160 wa mafunzo ya matayarisho (*pre-entry programme*). Jadweli namba 28 inatoa ufafanuzi zaidi.

Chuo kina wahadhiri 39 wazalendo na 7 kutoka nchi za nje. Wahadhiri saba wazalendo wamepelekwa masomoni katika vyuo mbali mbali duniani katika kiwango cha shahada za uzamivu (*PhD*). Vile vile jitihada zinaendelea kuwapeleka wahadhiri wengine masomoni kwa lengo la kukiwezesha chuo kujitosheleza kwa wahadhiri wake.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, chuo kitaanzisha mafunzo ya shahada ya uzamili katika uongozi wa umma. Pia, kinatarajiwa kuanza kutoa mafunzo ya shahada za kwanza katika mawasiliano ya simu (*Telecommunication Engineering)* na Kompyuta (*Computer Engineering*) baada ya kufunguliwa kwa Kitivo cha Uhandisi.

Aidha, chuo kitaendelea na mafunzo ya ngazi ya stashahada, lengo kuu likiwa ni kuwawezesha vijana ambao hawakupata sifa za moja kwa moja kujiunga na chuo katika kiwango cha shahada kuweza kupata fursa hiyo baada ya kufaulu katika kiwango cha stashahada. Utoaji wa stashahada hizo umezingatia vitivo viliopo chuoni, ili fursa hiyo iweze kutumiwa na kila mwanafunzi wa stashahada kuweza kujiunga na kitivo anachotaka. *(Makofi)*

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU CHUKWANI:

Mhe. Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu kiliopo Chukwani kinazidi kuimarika katika nyanja mbali mbali. Hadi kufikia Machi 2012, chuo kina jumla ya wanafunzi 1,210 wakiwemo wanawake 626 sawa na asilimia 52 ya

wanafunzi wote. Wanafunzi hawa wanasoma Shahada ya Kwanza ya Ualimu (88) na wengine wako katika mafunzo ya matayarisho (*pre-entry program*) ya kujiunga na shahada ya kwanza (322). Jadweli Namba 27 inatoa ufafanuzi zaidi. *(Makofi)*

Chuo pia kinaendelea na ujenzi wa madarasa na ofisi ya ghorofa moja ambayo ipo katika hatua za mwisho za kukamilika ambazo zitagharimu shilingi 1,017,000,000/=. Ujenzi wa nyumba za kukaa wafanyakazi umo katika hatua nzuri.

Mhe. Spika, Chuo kimetoa wahitimu 219 wakiwemo wanawake 78 na wanaume 141 katika mahafali ya 11 yaliyofanyika tarehe 25/1/2012 ambapo Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi alikuwa mgeni rasmi. Chuo hivi sasa kinakamilisha taratibu za usajili ili kiweze kuwa ni Chuo Kikuu kamili badala ya kuwa ni tawi la Chuo Kikuu chengine. Taratibu hizo zitakapokamilika chuo kitajulikana kwa jina la Chuo Kikuu cha Kimataifa za Zanzibar (*Zanzibar International University*) na kitatoa mafunzo katika nyanja nyengine mbali mbali. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kinatarajia kusajili wanafunzi wapya 600 wa fani mbali mbali na kuajiri wahadhiri saba ili kuondosha tatizo la kutumia wahadhiri wa muda. Aidha kiwanda cha Uchapishaji kitaendelea na kazi zake za kuhudumia jumuia ya chuo na taasisi nyengine za Serikali na binafsi. Ili kufanikisha azma hiyo Chuo kinatarajia kutumia Tsh 100,000,000/- ili kuweza kununua mitambo ya kisasa kwa ajili ya kiwanda chake. Chuo kimeshakamilisha taratibu za kuwa na tovuti yake ambayo inatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni.

Bodi ya Milopo ya Elimu ya Juu

Mhe. Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeanzishwa kwa sheria mpya namba 3/2011 ilioanza kutumika rasmi mwezi wa Julai 2011. Bodi imepewa majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi na wafanyakazi mbali mbali wanaojiunga na vyuo vya Elimu ya Juu. Aidha Bodi ina jukumu la kukusanya madeni yanayotokana na mikopo iliyotolewa na uliokuwa Mfuko wa Elimu ya Juu kuanzia mwaka 2006 pamoja na kutafuta nafasi za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Bodi imetayarisha na kuanza kutumia kanuni inayofafanua utekelezaji wa vifungu mbali mbali vya sheria hii mpya. Bodi ilitengewa jumla ya Tsh 4,000,000,000/- kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wapya na wale wanaoendelea. Hadi mwezi Juni 2012, fedha hizo zimeweza kupatikana zote kutoka mfuko mkuu wa Serikali. Jumla ya

wanafunzi wapya 209 sawa na asilimia 84 ya lengo waliteuliwa na kupatiwa mikopo na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wote waliohudumiwa kwa mikopo kwa mwaka 2011/2012 kufikia 1,086. Jadweli Namba 25(a) na 25(b) zinatoa ufafanuzi zaidi.

Hata hivyo mahitaji halisi ya fedha yalikuwa ni Tsh. 5.2 billioni na hivyo Bodi inakabiliwa na deni la ada ya vyuo mbali mbali na posho za utafiti za wanafunzi linalofikia jumla ya Tsh 1.2 billioni kwa mwaka uliopita. Pia, Bodi ya mikopo iliweza kukusanya madeni ya wanafunzi na jumla ya Tsh 8,200,000/= zimekusanywa kwa kipindi cha muda wa miezi mitatu kutoka kwa wanafunzi 71. Bodi inaendelea kuwafuatilia wanafunzi wengine waliokopeshwa ambao wamemaliza masomo yao ili nao waanze kulipa madeni yao. Katika kipindi hiki, wanafunzi 353 wamemaliza masomo yao na wanatarajiwa kurejea masomoni kutoka katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Bodi inatarajia kupeleka masomoni wanafunzi wapya 800 kwa kiwango cha shahada ya kwanza na shahada ya uzamili katika vyuo vya ndani ya nchi. Wanafunzi watateuliwa kwa mujibu wa fani zilizopewa vipaumbele kulingana na mahitaji ya soko la ajira ili wanaokopeshwa waweze kuajiriwa mara tu watapomaliza masomo na kuanza kurejesha mikopo yao. Tayari Serikali imekamilisha utafiti wa mahitaji katika fani mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Bodi imepangiwa ruzuku ya Tsh 8,000,000,000/- kwa ajili ya kuwadhamini wanafunzi wanaoendelea, wanafunzi wapya na kulipa madeni ya nyuma ya ada za wanafunzi.

Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu

Mhe. Spika, Baraza hili lina majukumu ya kusimamia shughuli zote zinazohusu mitihani ya SMZ ikiwemo utungaji, uchapishaji, usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba, kidato cha pili na mafunzo ya Ualimu (Stashahada ya msingi na Stashahada ya Dini ya Kiarabu). Pia Baraza lina jukumu la kutathmini mwenendo mzima wa malengo ya utowaji elimu pamoja na kutathmini mwenendo wa mitihani hiyo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2012, Baraza lilisimamia mwenendo mzima wa ufanyaji wa mitihani ya SMZ ambapo jumla ya skuli za msingi 225 (141 Unguja, 84 Pemba) zilifanya mitihani ya darasa la saba na skuli 186 (113 Unguja, 73 Pemba) zilifanya mitihani ya kidato cha pili. Jumla ya wanafunzi 23,798 walifanya mtihani wa darasa la saba katika mwezi Novemba 2011, kati yao wanafunzi 927 walichaguliwa kuingia madarasa ya kipawa na mchepuo.

Wanafunzi waliobakia wanaendelea na masomo yao katika madarasa ya kawaida ya kidato cha kwanza. Wanafunzi waliochaguliwa kuingia madarasa ya vipawa na michepuo ni sawa na asilimia 4.0 ya watahiniwa wote. Kwa upande wa mtihani wa kidato cha pili, kati ya wanafunzi 19,666 waliofanya mtihani, wanafunzi 11,041 ikiwa ni sawa na asilimia 56.1 walifaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha tatu katika skuli mbali mbali. Kiwango cha ufaulu kimeshuka ikilinganishwa na matokeo ya 2010 ambapo asilimia ya ufaulu ilifikia 58.2. Jadweli Namba 19 na 32 zinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa mitihani ya Taifa wa kidato cha nne, kati ya wanafunzi 11,877 wa skuli za Serikali na binafsi waliofanya mtihani huo mwezi wa Oktoba 2011, wanafunzi 9,020 wamefaulu ikiwa ni sawa na asilimia 75.9. Kiwango hiki cha ufaulu kimepanda ikilinganishwa na matokeo ya 2010 ambapo asilimia ya ufaulu ilifikia 71.7 Aidha, kati ya wanafunzi waliofaulu 1,270 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika skuli za Serikali mwaka 2012/2013, wakiwemo wanafunzi 718 kutoka skuli za Serikali, 90 wa skuli za binafsi na 462 wanafunzi wa faragha. Jadweli Namba 33a (i-ii) na 33b (i-ii) zinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, kati ya wanafunzi 1,813 waliofanya mtihani wa kidato cha sita mwezi Februari, 2012 wanafunzi 1,341 sawa na asilimia 74.0 walifaulu. Kiwango hiki cha ufaulu kimeshuka ikilinganishwa na matokeo ya Februari 2011 ambapo asilimia ya ufaulu ilikuwa 77.4. Jadweli Namba 34 inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa mitihani ya Ualimu, kati ya wanafunzi 100 waliofanya mtihani wa Stashahada ya Ualimu (sekondari) katika Chuo cha Kiislamu Mazizini na Chuo cha Kiislamu Kiuyu Pemba, wanafunzi 22 sawa na asilimia 22.0 walifaulu na wanafunzi 52 wamerudia mitihani yao. Aidha kati ya wanafunzi 78 waliofanya mtihani wa Stashahada ya Ualimu msingi katika Chuo cha Kiislamu, Mazizini na Benjamin William Mkapa, wanafunzi 49 sawa na asilimia 63 wamefaulu na wanafunzi 29 wamerudia mitihani yao.

Mhe. Spika, Jumla ya watahiniwa 3,301 wa Mtihani wa Kidato cha nne mwaka 2011 wamefutiwa matokeo yao kutokana na udanganyifu. Kwa upande wa Zanzibar, watahiniwa 1,020 wa skuli za serikali na binafsi walifutiwa matokeo na watahiniwa wa kujitegemea 1,056 wamefutiwa matokeo katika vituo 36 vya kufanyia mtihani, Unguja na Pemba. Uchunguzi uliofanywa na Wizara ulibaini kuwa kweli watahiniwa waliofutiwa matokeo yao walihusika na vitendo vya udanganyifu kwa njia moja au nyengine. Zaidi ya kufutiwa matokeo yao, Baraza la Mitihani la Tanzania limewaadhibu wote

waliofutiwa mitihani kutoruhusiwa kurudia mitihani kwa muda wa miaka mitatu. Hata hivyo, adhabu hiyo imepunguzwa na wanafunzi wameruhusiwa kurudia mitihani baada ya mwaka mmoja. Hatua hiyo imekuja baada ya mazungumzo kati ya Viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Tanzania Bara na Wizara yangu.

Kutokana na kitendo hicho, Wizara imewaandikia barua baadhi ya wasimamizi wa mitihani ya kuwataka watoe maelezo juu ya kukiukwa kwa taratibu za kufanya mitihani katika vituo walivyosimamia. Pia, Wizara imelitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kutopelekwa Baraza la Mitihani kwa majibu ya watahiniwa wa Somo la *"Fine Art"* wa skuli tatu za binafsi za Mkoa wa Mjini/Magharibi na kuagiza watakaobainika kufanya uzembe wafikishwe katika vyombo vya sheria. Wasimamizi wote watakaobainika kuwa walifanya uzembe katika kusimamia mitihani ya Kidato cha Nne, watachukuliwa hatua za kinidhamu.

Pamoja na hatua hizo, Wizara imeamua kuanzia mwaka 2012/2013, mitihani yote ya Taifa ya Kidato cha Nne, Sita na Ualimu ambayo inaendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania itaratibiwa kwa karibu na Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu badala ya Kamati za Mitihani ya Mikoa. Hatua hiyo itasaidia kuimarisha usimamizi katika mitihani ambao umeonekana kushuka sana. Pia Wizara itawahamasisha wazazi, wanafunzi na walimu ili kupiga vita vitendo vya udanganyifu katika mitihani ambavyo vinaonekana kushamiri sana.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lina lengo la kuandaa kanuni mbali mbali za ufanyaji na usimamizi wa mitihani ya SMZ. Pia inakusudia kuweka kumbukumbu zote za wanaotarajiwa kufanya mtihani katika mfumo wa kompyuta na kuongeza udhibiti wa mitihani hiyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, Baraza limetengewa ruzuku ya Tsh. 1,564,000,000/- kwa kazi za kawaida.

Bodi ya Huduma za Maktaba

Mhe. Spika, Bodi ya Huduma za Maktaba ni chombo kinachotekeleza shughuli zake kupitia shirika la Huduma za Maktaba. Bodi imepewa jukumu la kutoa na kuendeleza huduma za maktaba visiwani Unguja na Pemba. Kazi kubwa ya Bodi ya Huduma za Maktaba ni kuhakikisha kwamba huduma za maktaba zinawafikia wananchi wote wa Zanzibar.

Uimarishaji wa Kada ya Ukutubi

Mhe. Spika, kada ya Ukutubi hapa Zanzibar inaendelea kukua kwa kasi tangu kufunguliwa kwa jengo jipya la Maktaba kuu Maisara. Idadi ya watumiaji

imeongezeka kutoka asilimia 42.4 mwaka 2010 hadi asilimia 53.7 mwaka 2011. Shirika limeweka mkazo kusambaza huduma bora kwa watumiaji wa Maktaba kwa rika zote walioko sehemu, zote za nchi mjini na vijijini, Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kuiendeleza kada ya ukutubi, Shirika lilianzisha mafunzo ya ukutubi kwa ngazi ya awali katika mwaka 2011. Ninafuraha kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba jumla ya wahitimu 32 wakiwemo 22 wanawake na 10 wanaume wamehitimu masomo yao katika ngazi hii na kutunukiwa vyeti.

Mhe. Spika, katika kuhamasisha watoto kuwa na hamu na kujenga tabia ya kujisomea, Shirika linaendelea na programu ya watoto kupitia skuli mbali mbali hususan skuli za msingi kwa Unguja na Pemba. Kuwepo kwa programu hiyo kumewapelekea watoto kuwa na mwamko wa kujisomea.

Mhe. Spika, Shirika linaendelea kupokea msaada wa vitabu kutoka "*Book Aid International*" ya Uingereza. Jumla ya skuli 25 za Unguja zimepatiwa vitabu kupitia mradi wa Maktaba za sanduku. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya skuli 10 za Wilaya ya Micheweni Pemba zinatarajiwa kupatiwa vitabu kupitia mradi huu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika hili limetengewa ruzuku ya Tsh. 297,000,000/- kwa kazi za kawaida.

Kitengo ya Uhasibu

Mheshimiwa Spika. Kitengo hiki kimekuwa kikishughulikia fedha zote zinazopokelewa Wizarani katika fungu la kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kwa mwaka 2011/2012, Kitengo kimesimamia ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na mahitaji mengine ya Wizara. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Kitengo kimesimamia ulipaji wa fedha za wakandarasi wa ujenzi na wazabuni wa vifaa na huduma mbalimbali. Kitengo kimekuwa na mashirikiano mazuri na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika matumizi ya mtambo wa IFMS ambao husaidia kwa kiwango kikubwa katika usimamizi wa matumizi kwa mujibu wa bajeti ya Wizara na udhibiti wa fedha za umma.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013, Kitengo kitaendelea kusimamia matumizi yote ya fedha za kawaida na fedha za maendeleo kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa. Aidha, Kitengo kinakusudia kutoa mafunzo kwa watumishi wake ili kuwaongezea uwezo ujuzi na ufanisi wake wa utendaji wao. Mafunzo haya yatalenga katika teknolojia ya kompyuta na uhasibu.

Kitengo cha Habaru Elimu na Uhusiano

Mhe. Spika, Kitengo cha Habari Elimu na Mahusiano katika Elimu kwa mwaka 2011/2012 kiliendelea kutekeleza majukumu ya kuratibu shughuli za Ofisi ya Waziri pamoja na Wizara kwa jumla. Miongoni mwa shughuli zilizofanikishwa ni kukuza na kuimarisha ushirikiano na nchi mbali mbali pamoja na Mashirika ya Kimataifa. Mafanikio haya yametokana na kukutana na Mabalozi wa nchi za nje waliopo Tanzania na Viongozi wa Mashirika ya Kimataifa. Viongozi wa Wizara pia walihudhuria katika mikutano na makongamano ya Kimataifa kuhusiana na elimu. Miongoni mwa Mabalozi wa nchi niliokutana nao ni kutoka nchi za China, Iran, Oman, Nigeria na India. Kwa upande wa Mashirika ya Kimataifa ni USAID, IDB (*Islamic Development Bank*), AfDB, UNICEF na Chuo Kikuu cha Taifa cha South Carolina (Marekani).

Aidha, miongoni mwa mikutano tuliyohudhuria ni mikutano iliyoandaliwa na "*The Association for the Development of Education in Africa*" – Ogaduague Bukinafaso, FAWE – Kenya, COMEDAF-V Abuja Nigeria, *Africa Council for Distance Education – Zanzibar* na 3rd *Annual International East African Linkage Conference on Special Needs – Zanzibar*. Mikutano hiyo imesaidia sana katika kuimarisha maendeleo yetu katika elimu. Katika kuimarisha Kitengo, wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo mafupi mjini Dar-es-salaam na India ili kuimarisha utendaji wao.

Kitengo cha Ununuzi na Ugavi

Mhe. Spika, Kitengo cha Ununuzi na Ugavi ambacho ndicho sekretariati ya Bodi ya Zabuni ya Wizara kinaendelea kufanya kazi zake vizuri. Katika mwaka 2011/2012, Kitengo kwa kushirikiana na Bodi ya Zabuni kilitayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini jumla ya zabuni 21 za manunuzi ya bidhaa, huduma na kazi za ujenzi zenye thamani ya jumla ya Tsh. 16,898,561,313/=

Miongoni wa fedha hizo, jumla ya Tsh. 5,595,198,061/= ni kwa ajili ya ujenzi wa skuli za ghorofa za Mpendae, Kwamtipura na Kiembesamaki ambazo zinagharamiwa na Benki ya Dunia na SMZ. Jumla ya Tsh. 6,235,514,520/- ni kwa ajili ya ukarabati wa skuli ya Forodhani, Hamamni, Tumekuja, Utaani, Fidel Castro na Uweleni. Jumla ya Tsh. 6,235,514,520/- ni kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma ambazo zimegharamiwa na SMZ, Benki ya Dunia, Badea, Sida na washirika mbali mbali wa maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Kitengo kinakusudia kutayarisha, kutangaza na kuzifanyia tathmini zabuni zinazohusiana na ununuzi wa samani kwa ajili ya skuli sita za sekondari zinazofanyiwa ukarabati na skuli tatu za Mjini Magharibi za Unguja za ghorofa zilizoanza kujengwa. Aidha Kitengo kinakusudia kutangaza zabuni za ununuzi wa vitabu vya wanafunzi na

miongozo ya walimu vya darasa 1 hadi 4, ununuzi wa samani kwa ajili ya skuli za msingi na sekondari, zabuni za kuwatafuta washauri waelekezi wa kusanifu majengo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vitatu vya elimu mbadala na vituo viwili vya mafunzo ya amali chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Pia inakusudia kutangaza zabuni ya upanuzi na ukarabati wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na upanuzi na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii cha Zanzibar na kukamilisha tathmini ya zabuni za wakandarasi wa ujenzi wa skuli mbili za sekondari za ghorofa za Kibuteni Unguja na Mkanyageni Pemba chini ya ufadhili wa Badea

Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani

Mhe. Spika, Kitengo hiki kina jukumu la kukagua hesabu zinazohusiana na matumizi pamoja na mapato katika Idara zote za Wizara hii. Pia Kitengo kinafanya ukaguzi wa kuangalia michango yote inayotolewa na wazee na wanafunzi kwa skuli zote za Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2011/2012, Kitengo kimeweza kukagua hesabu zote za fedha za kawaida na fedha za maendeleo kuanzia Makao Mkuu ya Wizara pamoja na kufuatilia vifaa vilivyopelekwa katika skuli mbali mbali ambavyo hununuliwa kutokana na bajeti husika ya mwaka wa fedha.

Pia fedha za miradi ya maendeleo kulingana na thamani halisi ya bidhaa zilizopokelewa na ujenzi uliofanyika. Aidha Kitengo kimeweza kuzifanyia ukaguzi skuli 82 zikiwemo 5 za maandalizi, 36 za msingi na 41 za sekondari. Kitengo pia kimefanya ukaguzi wa Taasisi nne ambazo hupatiwa ruzuku kutoka bajeti kuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Tasisi hizo ni Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia

Kitengo cha Ukaguzi pia kinaratibu na kuendesha vikao mbali mbali vya Kamati ya Ukaguzi – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (*Audit Committee*) kwa kuwasilisha ripoti mbali mbali za ukaguzi ili kuchangiwa na wajumbe wa kamati ya wakaguzi wa hesabu.

Mhe. Spika, Kitengo katika mwaka 2012/2013, kitaendelea kufanya ukaguzi wa mahesabu ya Idara zote za Wilaya ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Taasisi na skuli zake mbali mbali za Unguja na Pemba. Pia kitengo kitaendelea na utaratibu wake wa kutoa mafunzo ya uwekaji wa kumbukumbu za Hesabu na uwekaji wa rekodi za vifaa mafunzo ambayo huwashirikisha

wenyeviti wa Kamati za skuli, walimu wakuu wa skuli husika pamoja na washika fedha wa skuli ili kuwajengea uwelewa kuhusiana na kazi zao.

Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu

Mhe. Spika, Kitengo hiki kina jukumu la kuratibu maendeleo ya elimu ya juu na kuwa na mashirikiano ya karibu na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania, Vyuo vikuu vilivyoko Zanzibar na vilivyoko Tanzania Bara na taasisi nyengine za elimu ya juu. Katika mwaka 2011/2012, Kitengo hiki kilendelea na kazi zake kama kawaida za uratibu ikiwa ni pamoja na kutangaza nafasi za masomo zinazotolewa na Nchi/Mashirika mbali mbali kwa Tanzania. Katika mwaka 2012/2013, Kitengo kinatarajia kuendelea kuratibu utoaji mafunzo ya Elimu ya Juu, ili kuwapa fursa muhimu wanafunzi wa Kizanzibari. Aidha Kitengo kimekusudia kuendeleza mahusiano yake na Taasisi za Elimu ya Juu za Zanzibar na Tanzania Bara. Pia Kitengo kitaendelea na uwekaji wa kumbukumbu kwa wahitimu wanaorejea masomoni na pia kuwapatia barua ili wapeleke ofisi inayohusiana na Utumishi wa Umma kwa ajili ya kupatiwa ajira.

Kitengo cha Elimu Mjumuisho wa Stadi za Maisha

Mhe. Spika, Kitengo hiki kina jukumu la kusimamia na kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu, wakiwemo watoto wenye ulemavu na watoto walioko katika mazingira hatarishi wanapatiwa elimu iliyobora katika mazingira rafiki, kutoa ushauri nasaha, kusimamia mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, kuhamasisha wanafunzi wa kike kupenda kusoma na kuwapatia stadi za maisha walimu na wanafunzi.

Elimu Mjumuisho

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, Kitengo kimewahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu 4,500 kati yao wasichana ni 2,201 na wavulana 2,299 katika skuli 86 Unguja na Pemba. Wanafunzi wawili wa kike wamefaulu kuingia darasa la 9 la michepuo katika skuli ya Vikokotoni kutoka skuli ya Kisiwandui katika Mtihani wa darasa la saba mwaka 2011. Kitengo, pia kiliandaa upimaji wa wanafunzi. Jumla ya wanafunzi 696 (Wanawake 428, 268 Wanaume) wamegundulika kuwa na matatizo makubwa na wamepatiwa rufaa na kuhudhuria hospitali kuu ili kuchunguzwa zaidi. Katika suala la ufuatiliaji, jumla ya skuli 24 (15 Unguja, 9 Pemba) zilipitiwa na kuangaliwa utekelezaji wa programu za Elimu Mjumuisho inavyotekelezwa. Kwa kiasi kikubwa hali inaridhisha. Idadi ya watoto wenye mahitaji maalum wanaopelekwa skuli inazidi kuongezeka.

Mhe. Spika, Kitengo kilitoa mafunzo mbali mbali kwa walimu ili waweze kuwahudumia wanafunzi vizuri zaidi. Miongoni mwa mafunzo yaliyotolewa

ni pamoja na mafunzo juu ya lugha ya alama, maandishi na nukta nundu, dhamira ya elimu mjumuisho na mafunzo ya kompyuta (kwa walimu na wanafunzi wasioona), na ushauri nasaha. Jumla ya washiriki wa mafunzo 649 (356 wanawake, 293 wanaume) kutoka Unguja na Pemba walihudhuria mafunzo hayo. Pia, mikutano mbali mbali ya uhamasishaji ilifanyika. Mikutano hio ilihusisha wazazi wa watoto wenye mahitaji maalum, wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Zanzibar vikiwemo Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu.

Stadi za Maisha

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, mafunzo ya stadi za maisha kwa walimu 85 yametolewa Unguja na Pemba. Pia mafunzo juu ya utumiaji wa mwongozo wa kufundishia stadi za maisha kwa walimu wanaosomesha kidato cha tatu kwa masomo ya Kiingereza, Jiografia, Uraia na Biolojia yametolewa. Jumla ya walimu 500 wamepatiwa mafunzo hayo. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la UNICEF imefungua Klabu za Afya katika skuli 4 mpya za msingi Kisiwani Pemba. Skuli hizo ni Kunguni -Wilaya ya Mkoani, Pujini - Wilaya ya Chake Chake, Mjini Kiuyu - Wilaya ya Wete na Karume - Wilaya ya Micheweni. Walimu wakuu, walimu wa ushauri nasaha na viongozi wa Serikali za wanafunzi wa skuli hizo walipatiwa mafunzo ya stadi za maisha, uundaji na uendeshaji wa Klabu za Afya za skuli.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itaendeleza shughuli za ushauri nasaha, masuala ya jinsia na mapambano dhidi ya UKIMWI. Walimu watapatiwa mafunzo juu ya stadi za maisha na kufungua klabu za afya kwa skuli ambazo hazina klabu hizo. Pia, Kitengo kitaendelea na uhamasishaji wa jamii juu ya umuhimu wa elimu mjumuisho, itakamilisha rasimu ya sera ya elimu mjumuisho na miongozo yake na itaimarisha ushirikiano na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi. Aidha shughuli za upimaji wa wanafunzi, ushauri nasaha, masuala ya jinsia na mapambano dhidi ya UKIMWI yataendelezwa.

KITENGO CHA URAJIS

Kesi za Ardhi

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Kitengo cha Urajis wa Elimu kimeshughulikia kesi moja ambayo inahusiana na kuvamiwa kwa eneo la skuli ya Welezo. Kesi hii ilianza mwaka 2007, katika Mahkama ya Ardhi na Wizara bado inaifuatilia kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Leseni za Walimu

Mhe. Spika, Jumla ya walimu 362 walipatiwa leseni za kusomeshea katika skuli za Serikali na skuli za binafsi. Kati yao walimu 228 waliosomea na walimu 134 wasiosomea walipatiwa leseni. Pia maafisa wa Kitengo walifuatilia skuli mbali mbali za Serikali na za binafsi kuhakikisha kama walimu wao wana leseni. Katika mwaka 2012/2012, Ofisi ya Mrajis itaendelea kutoa leseni za walimu wapya na walimu ambao leseni zao zimepitwa na wakati.

Maombi ya Usajili wa Skuli za Binafsi

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, maombi 7 ya usajili wa skuli za Serikali na skuli 28 za binafsi yalipokelewa. Skuli zote 7 za Serikali zilipata usajili na skuli 9 za binafsi pia zilipewa usajili baada ya kufanyiwa ukaguzi. Kwa mwaka 2012/2013, Kitengo cha Urajis wa Elimu kitaendelea kushughulikia maombi ya usajili wa skuli za Serikali na binafsi.

KESI ZA UJAUZITO WA NDOA ZA WANAFUNZI

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, kesi 28 za ndoa za wanafunzi ziliripotiwa na kesi 3 kati ya hizo zilikuwa baina ya wanafunzi kwa wanafunzi. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Nambari 6 ya mwaka 1982 kifungu 20 (3) wanafunzi 18 walifukuzwa skuli. Pia, kesi 15 za ujauzito za wanafunzi ziliripotiwa ambapo kesi mbili zilikuwa za wanafunzi kwa wanafunzi. Kesi 9 kati ya hizo zilijadiliwa katika Afisi ya Mrajis wa Elimu na mwanafunzi mmoja anaendelea na masomo na wanafunzi 8 wamekubali kuendelea na masomo baada ya kukamilisha taratibu. Katika mwaka 2012/2013, Kitengo kitaendelea kushughulikia kesi za ujauzito wa wanafunzi kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya mwaka 2005 ya kuwalinda wari na watoto wa mzazi moja. Pia kitaendelea kushughulikia kesi za ndoa za wanafunzi kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 6 ya mwaka 1982.

Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya

Mhe. Spika, Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya zinaendelea na taratibu za uteuzi wa wajumbe wapya na zitaanza vikao vyake mara baada ya uteuzi kukamilika.

Baraza la Elimu

Mhe. Spika, Baraza la Elimu limeundwa upya hivi karibuni baada ya wajumbe wa Baraza lililopita kumaliza muda wake. Uzinduzi wa Baraza hilo umefanyika hivi karibuni na Baraza linaendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

KITENGO CHA MICHEZO NA UTAMADUNI

Mhe. Spika, Kitengo hiki kina majukumu ya kutekeleza Sera ya Taifa ya michezo ndani ya skuli kwa kuandaa na kukuza vipaji vya watoto ambao wanatarajiwa kuwa wanamichezo muhimu wa taifa letu kwa siku zijazo. Pia, kuwaandaa wanafunzi kwa wenye kiwiliwili chenye afya njema na kuwasaidia katika masomo yao.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Kitengo cha Michezo na Utamaduni kimeendeleza michezo mbali mbali katika skuli zetu. Kitengo kimeandaa mafunzo mbali mbali ya michezo kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazojishughulisha na michezo hapa Zanzibar na Tanzania kwa jumla. Miongoni mwa taasisi hizo ni pamoja na Chama cha Kriket cha Tanzania kwa kushirikiana na shirikisho la Afrika kupitia BTMZ ambao iliwapatia walimu mafunzo ya mchezo huo ili kuibua, kuinua na kurejesha hadhi ya mchezo huo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Pia, Kitengo kwa kushirikiana na Taasisi ya "*International Education and Sport Consultants (IESC)"* ya Marekani iliendesha mafunzo ya mpira wa wavu kwa walimu 40 kutoka katika skuli mbali mbali za hapa Unguja. Mafunzo kama hayo yanatarajiwa kutolewa huko Pemba sambamba na mafunzo ya mpira wa kikapu katika mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Kitengo kiliandaa na kutoa mafunzo kwa walimu wa skuli za msingi wanaofundisha somo la michezo kwa darasa la kwanza na la pili katika Wilaya sita (6) za Unguja na Pemba kwa mujibu wa muhutasari wa somo hilo ambao hivi sasa unatumika hadi darasa la tatu. Katika mafunzo hayo jumla ya walimu 159 wa madarasa hayo walipatiwa mafunzo ambayo yatawasaidia kupata mbinu mbali mbali za kufundisha somo hilo kwa ufanisi. Mafunzo hayo yaliendeshwa kupitia vituo vya walimu katika Wilaya ya Kusini, Kati, Kaskazini "A", Chake chake, Wete, Mjini na Wilaya ya Magharibi. Aidha, mafunzo kwa walimu kwa vituo vya Wilaya ya Magharibi, Kaskazini "B", Mkoani na Micheweni yatatolewa katika mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, Timu zetu zilishiriki katika mashindano ya UMISSETA yaliyofanyika huko Kibaha Tanzania Bara hivi karibuni. Timu zetu ziliweza kupata ushindi wa kwanza katika mchezo wa mpira wa miguu, ushindi wa pili katika mpira wa meza - wanaume, ushindi wa tatu katika mpira wa mikono - wanaume, na mshindi wa tatu katika mpira wa kikapu - wanawake. Aidha, mwanafunzi Ibrahim Hamad Hilika wa Skuli ya Sekondari ya Kwamtipura amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mpira wa miguu katika mashindano hayo. Pia, Kitengo chetu, kimefanya marekebisho ya mwongozo unaosimamia

michezo na kuandaa mwongozo mpya ambao utawezesha kutoa muelekeo wa uendeshaji wa michezo katika skuli zetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kitengo kitaandaa mafunzo mbali mbali ya michezo kwa skuli zetu za Unguja na Pemba kwa kushirikiana na taasisi nyengine za michezo ndani na nje ya nchi yetu kadiri hali ya kifedha itakavyoruhusu. Pia, kwa kushirikiana na Kamati ya Olimpiki ya Tanzania na "*British Council*" Kitengo kimedhamiria kuendesha mafunzo ya michezo mbali mbali sambamba na ile ya asili katika maeneo ya Dole Wilaya ya Magharibi Unguja kwa majaribio ya awali.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2012/2013, Kitengo kitaendelea na utaratibu wa kuandaa sherehe za Tamasha la Elimu bila ya malipo kuanzia ngazi ya skuli, kanda, wilaya, mkoa hadi Taifa. Pia kuendelea kushiriki na kushindana katika michezo na sanaa kwa skuli za sekondari Tanzania (UMISSETA) na ile itakayoandaliwa na Shirikisho la FEASSA kwa Afrika Mashariki inayofanyika kila mwaka kwa lengo la kuendelea kuibua, kuinua na kuendeleza vipaji vya vijana wetu na kuitangaza Zanzibar kupitia midani za michezo nje ya mipaka yake.

MAPATO

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya Tsh. 15,000,000/- kutoka vianzio vya ada za leseni za walimu pamoja na uandikishaji wa skuli binafsi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, jumla ya Tsh. 8,520,800/= zilikusanywa na kuwasilishwa ikiwa sawa na asilimia 57.0 ya makadirio. Kupungua kwa makusanyo kunatokana na idadi ndogo ya walimu wapya walioajiriwa na viwango vidogo vya leseni za walimu. Katika mwaka 2012/2013, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakusudia kukusanya jumla ya Tsh. 22,500,000/- ikiwa ni mapato ya usajili wa skuli za binafsi na leseni za walimu na kuziwasilisha hazina.

JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika, Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Tsh. 110,091,291,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 71,050,000,000/- ni kwa matumizi ya kawaida, Tsh. 5,100,000,000/- za SMZ na Tsh. 33,869,291,000/- za washirika wa maendeleo. Jadweli Namba 46 na 47 zinatoa uchambua zaidi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru kwa kutumia muda wa saa 2.40 kuwasilisha hotuba zaidi ya saa 2 ziliomo ndani ya Kanuni. Waheshimiwa walikuvumilia kwa sababu ya usomaji wa taratibu ili kuona kila Mheshimiwa mjumbe anafahamu vizuri kile kilichomo ndani ya hotuba hii. Hoja imeungwa mkono waheshimiwa wajumbe mtajadili jioni.

Naomba sasa niakhirishe kikao hiki hadi saa 11.00 jioni leo.

(7.00 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

TAARIFA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe taarifa kwamba tumepokea habari ya matatizo ya meli na hivi sasa viongozi wetu wote wa kitaifa wako Bandarini na wanatizama hali ilivyo kuweza kutoa msaada, sasa na sisi tumetakiwa tuungane nao ili tuweze kuona yaliyotokea tusaidiane. Sasa namuomba Mwanasheria Mkuu atoe hoja ya kuakhirisha kikao na baadae niakhirishe kikao hadi kesho.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya dharura ya kitaifa iliyotokea na ambapo Baraza limepata taarifa na wewe mwenyewe Mhe. Naibu Spika, umetupa taarifa hiyo, na kwa kuwa bado kuna hoja ambayo iko mbele yetu na haijamaliza kujadiliwa, na kwa sababu muda wa kuakhirisha Baraza bado hujafika naomba Baraza lako tukufu litenge kando kanuni ya muda na Baraza letu liweze kuakhirishwa kabla ya muda wake ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wapate fursa ya kuungana na viongozi na wananchi wengine katika dharura hii ya kitaifa. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Niwahoji waliokubaliana na hoja. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 11:02 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 19/07/2012 saa 3:00 asubuhi)